Toleo Na. 1 | Januari - Juni, 2023

HALIUZWI

# JARIDA LA MASHTAKA

## HAKI, AMANI NA USALAMA KWA MAENDELEO YA TAIFA



Muonekano wa Jengo la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka linalojengwa Njedengwa Jijini Dodoma.




Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Sylvester Antony Mwakitalu kuwa Mkurugenzi wa Mashtaka.

Ofisi_ya_taifa_ya_mashtaka_tz Omashtaka Mashtaka tv Email: dpp@nps.go.tz www.nps.go.tz

# BODI YA UHARIRI


| | |
|---|---|
| **Mwenyekiti** | **Sylvester Anthony Mwakitalu**<br>Mkurugenzi wa Mashtaka |
| **Makamu Mwenyekiti** | **Joseph Sebastian Pande**<br>Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka |
| **Mhariri Mkuu** | **Rebecca Kwandu**<br>Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini |

**Tumaini Kweka**
Mkurugenzi Divisheni ya Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi

**Oswald Tibabyekomya**
Mkurugenzi Divisheni ya Makosa ya Udanganyifu, Utakatishaji Fedha na Rushwa

**Neema Mwanda**
Mkurugenzi Divisheni ya Usimamizi wa Kesi na Uratibu wa Upelelezi

**Faraja Nchimbi**
Kaimu Mkurugenzi Divisheni ya Utaifishaji Mali na Makosa Yanayovuka Mipaka

**Shedrack Kimaro**
Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utaifishaji na Urejeshaji Mali

**Pendo Makondo**
Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi

**Zamaradi Kawawa**
Mkurugenzi kutoka Idara ya Habari Maelezo

**Marygoreth Ntandu**
Afisa Habari

**Henry Mwakigali**
Afisa TEHAMA

Msanifu wa Jarida: Afisa TEHAMA

# Tahariri ya Mhariri

Napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha kusoma toleo la Kwanza la Jarida la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ambalo ni la Kwanza tangu ilipogawanya na kuwa Ofisi huru yenye Mamlaka kamili ya kujiendesha kikatiba katika suala zima la uendeshaji wa Kesi za Jinai nchini.

Jarida hili limelenga katika kuwaelimisha wasomaji juu ya historia ya kuanzishwa kwa ,Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Muundo wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuanzia ngazi ya Makao Makuu, Mkoa na Wilaya pamoja na kuelimisha juu ya Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Katika kuelimisha juu ya Muundo wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Jarida linaelimisha juu ya Muundo na Majukumu ya kila Divisheni na Vitengo, Muundo wa Mikoa na Wilaya pamoja na majukumu yake, pia litaonyesha namna Muundo huo unavyofanya kazi zikiwepo sehemu za taasisi pamoja na picha za Viongozi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika ngazi za Makao Makuu na Mikoa.

Aidha, tutapata nafasi ya kusoma/ kupata neno kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka na Msaidizi wake, litakuletea utani mbalimbali unaotokea mahakamani kwa lengo la kukufurahisha na kukupa tabasamu murua, litakuletea habari motomoto ya masuala ambayo ulitakiwa kuyafahamu (Did You Know) na pia litakuelimisha na kukuhabarisha juu ya Mafanikio ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka toka kuanzishwa kwake mwaka 2018.

Katika Jarida hili pia utapata anuani Muhimu za Watendaji wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuanzia ngazi



**Rebecca Kwandu**

**Mhariri Mkuu**

ya Taifa, Mikoa hadi Wilaya ambazo zitakusaidia kuwasiliana bila shida pale utakapohitaji.

Pia utaona picha mbalimbali ya matukio ya habari na picha ambazo zinaonyesha shughuli mbalimbali zilizotekelezwa na Ofisi ya Taifa na Mashtaka.

Napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha kwa moyo Mkunjufu kulisoma Jarida hili na kulitumia kama rejea pale unapohitaji kufanya rejea katika masuala ya kitaaluma.

Ni imani yangu kuwa habari, makala na picha zilizopo katika jarida hili zitakupa hamasa za kuzisoma na kutoa maoni yako ya kuboresha kwa ajili ya makala zijazo.

# Neno Kutoka kwa Mwenyekiti wa Bodi ya Uhariri

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (OTM) imekuwepo kufuatia mabadiliko ya muundo wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yaliyofanyika Februari, 2018, kwa Hati idhini ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Tangazo la Serikali Namba 49 la mwaka 2018 na kuifanya iliyokuwa Divisheni ya Mashtaka chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuwa Ofisi huru inayojitegemea na yenye Mamlaka kamili. Lengo la mabadiliko haya ilikuwa ni kuongeza ufanisi na tija katika kuratibu shughuli za upelelezi zinazofanywa na vyombo chunguzi na uendeshaji wa kesi za jinai.

Katika kutekeleza majukumu yake, OTM inaongozwa na Dira isemayo Haki, Amani na Usalama kwa Maendeleo ya Taifa. Ili kutekeleza Dira hii, OTM imejiwekea Dhima inayotaka tufanye kazi na wadau na kuendesha kesi bila woga au upendeleo ili kuhakikisha Haki, Amani na Usalama vinatawala katika jamii.



**Sylvester Anthony Mwakitalu**

**Mkurugenzi wa Mashtaka**

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mashtaka ya mwaka 2008 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 2 ya mwaka 2018, OTM inatakiwa kutoa taarifa za utekelezaji wa majukumu yake kwa Waziri wa Katiba na Sheria.

Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Watumishi wa OTM, Wadau wa Haki Jinai na wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano walioutoa katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yetu.

Napenda pia kuwakaribisha watu wote kulisoma Jarida la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili kujifunza na kufahamu majukumu ya Ofisi hii ili kwa pamoja tushirikiane kuhakikisha Haki, Amani na Usalama vinatawala nchini

**Haki, Amani na Usalama Kwa Maendeleo ya Taifa**

# Kona ya Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka



**Joseph Sebastian Pande**

**Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka**

Napenda kuchukua nafasi hii kuwashukuru Menejimenti na Watumishi wote wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kuiwezesha Bodi ya Uhariri wa Jarida la Mashtaka kuandaa toleo hili la kwanza tangu kuanzishwa kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Napenda pia kuwakaribisha wadau na watanzania wote kwa ujumla kulisoma Jarida la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ili kujifunza na kufahamu majukumu yanayotekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Natoa wito kwa Menejimenti na watumishi wote wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kushirikiana na Bodi ya Uhariri wa Jarida la Mashtaka kufanikisha uandaaji wa Jarida kwa kuandika makala ili kufanikisha utokaji wa Matoleo yajayo ya jarida letu.

Ushirikiano imara katika utekelezaji wa majukumu yetu ndio ngao imara ya kufanikisha Dira na Dhima ya Ofisi yetu. Kila mmoja kwa upande wake na nafasi yake ajitahidi kufanya kazi kwa juhudi na maarifa ili tuweze kufikia malengo tuliyojiwekea.

Nikiwa Afisa Masuuli Mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka nitaendelea kuwezesha upatikanaji wa rasilimali fedha ili kuhakikisha jarida hili linatoka kwa wakati.

Tushirikiane kwa pamoja kuhakikisha kuwa Dira ya Ofisi yetu inatekelezwa ili kuwezesha upatikanaji wa Haki, Amani na Usalama kwa Maendeleo ya Taifa

# Je Wajua?

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeanzishwa kama Ofisi huru ya Umma kupitia Tangazo la Serikali Na.49 la mwaka 2018 la tarehe 13 Februari, 2018. Lengo la kuanzisha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni kutekeleza mamlaka ya Kikatiba aliyopewa Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye anatoa mchango mkubwa katika kusimamia Haki Jinai kwa mujibu wa Ibara ya 59B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977.

Kwa msingi huo, Mkurugenzi wa Mashtaka ana uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka yote ya jinai nchini. Kutokana na Ibara hiyo ya Katiba, Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Mashtaka hayamhusu mtu mwingine yoyote au mamlaka nyingine na hawajibiki kusimamiwa na mtu mwingine yoyote au mamlaka nyingine.

Katika kutekeleza majukumu yake, Mkurugenzi wa Mashtaka anatakiwa kufuata kanuni ya kutenda haki na kuzuia ukiukaji wa taratibu za kisheria na maslahi ya umma. Nafasi hii imewekwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430.

Tangazo la Serikali Na.49 la mwaka 2018 limeweka mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, muundo wake, utawala, ufuatiliaji, usimamizi wa mashtaka na namna uratibu wa upelelezi utakavyokuwa kwa lengo la kukuza na kuinua utendaji haki jinai na masuala yanayohusiana nayo.

Hivyo basi fahamu kuwa, Mkurugenzi wa Mashtaka amepewa uwezo na mamlaka ya kusimamia uendeshaji wa mashtaka yote ya jinai katika Mahakama zote nchini isipokuwa Mahakama za Kijeshi.

# Yaliyomo




**Ifahamu Ofisi ya Taifa ya Mashtaka** Uk. 07

Uk. 58 **Utaifishaji na Urejeshaji wa Mali Zitokanazo na Uhalifu**

Uk. 64 **Ulinzi wa Mashahidi Katika Mfumo wa Haki Jinai**

Uk. 67 **Ijue Sheria na Miongozo ya Maamuzi ya Kushtaki**

Uk. 73 **Dhamana Katika Jinai**

Uk. 77 **Utani wa Kisheria**



# IFAHAMU OFISI YA TAIFA YA MASHTAKA

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka,
Chuo cha Masomo ya Biashara na Sheria cha Chuo Kikuu cha Dodoma- UDOM,
S.L.P 1733, Dodoma, Tanzania.
Simu: +255 26 2963634, Nukushi: +255 26 2963635
Simupapo: +255 26 2963634, Barua Pepe: dpp@nps.go.tz.

# UTANGULIZI

*Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeanzishwa kama Ofisi huru ya Umma kupitia Tangazo la Serikali Na. 49 la mwaka 2018 la tarehe 13 Februari, 2018 la kuanzisha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa ajili ya kutekeleza mamlaka ya Kikatiba aliyopewa Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye anatoa mchango mkubwa katika kusimamia haki jinai. Kwa mujibu wa Ibara ya 59B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, Mkurugenzi wa Mashtaka amepewa uwezo na mamlaka ya kusimamia uendeshaji wa mashtaka yote ya jinai katika Mahakama zote isipokuwa mahakama za kijeshi. Kwa msingi huo, Mkurugenzi wa Mashtaka ana uwezo wa kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka yote ya jinai nchini.*

*Kutokana na Ibara hiyo ya Katiba, Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Mashtaka hayamhusu mtu mwingine yoyote au mamlaka nyingine na hawajibiki kusimamiwa na mtu mwingine yoyote au mamlaka nyingine.*

*Katika kutekeleza majukumu yake, Mkurugenzi wa Mashtaka anatakiwa kufuata kanuni zifuatazo: Kutenda haki; Kuzuia ukiukaji wa taratibu za kisheria; na maslahi ya umma. Nafasi hii imewekwa chini ya kifungu cha 8 cha Sheria ya Taifa ya Mashtaka, Sura ya 430.*

*Tangazo la Serikali Na.49 la mwaka 2018 limeweka mpangilio wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, muundo wake, utawala, ufuatiliaji usimamizi wa mashtaka na namna uratibu wa upelelezi utakavyokuwa kwa lengo la kukuza na kuinua utendaji haki jinai na masuala yanayohusiana nayo.*




*Uzinduzi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Jengo la UDOM Jijini Dodoma*

## DIRA

## DHIMA

**Haki, Amani na Usalama kwa Maendeleo ya Taifa**

**Kushirikiana na wadau na kuendesha kesi bila woga, upendeleo ili kuhakikisha uwepo wa haki, amani, na usalama katika jamii**

## MAADILI YA MSINGI

**Uwajibikaji:** kuwajibika katika utekelezaji wa majukumu kwa wakati;

**Kukubalika:** uthabiti na uwezo wa kuaminika na kuthaminiwa;

**Uadilifu:** kwa maadili na uaminifu bila kuvumilia vitendo vya rushwa na ubadhirifu;

**Uweledi:** kwa kujituma, kujitoa, umahili na utaalamu ndani na nje ya ofisi;

**Huduma bora:** kwa kutoa huduma bora kwa kufanya kazi pamoja, heshima na adabu.

# DIVISHENI NA VITENGO KATIKA Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

## DIVISHENI

- Divisheni ya Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi
- Divisheni ya Utaifishaji Mali na Makosa yanayovuka Mipaka
- Divisheni ya Usimamizi wa Kesi na Uratibu wa Upelelezi
- Divisheni ya Makosa ya Udanganyifu, Utakatishaji Fedha na Rushwa
- Divisheni ya Utawala na Rasilimali Watu
- Divisheni ya Mipango

## VITENGO

- Kitengo cha Huduma ya Utafiti na Maktaba
- Kitengo cha Masjala ya Sheria
- Kitengo cha Ununuzi na Ugavi
- Kitengo cha Uhasibu na Fedha
- Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani
- Kitengo cha TEHAMA
- Kitengo cha Mawasiliano Serikalini



# Majukumu ya Mkurugenzi wa Mashtaka

## Bw. Sylvester Anthony Mwakitalu

Mkurugenzi wa Mashtaka ni mkuu wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka. Mkurugenzi wa Mashtaka ndiye Msimamizi Mkuu wa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, Wakurugenzi, Wakurugenzi Wasaidizi, Mawakili wa Serikali na Waendesha Mashtaka katika kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

## MAJUKUMU

Kuamua kushtaki au kutoshtaki kwenye makosa ya jinai;

Kuanzisha, kuendesha na kusimamia mashtaka ya makosa ya jinai katika mahakama zote isipokuwa mahakama za kijeshi;

Kutwaa na kuendelea na mashtaka ya kesi yoyote ya jinai iliyofunguliwa na mtu au taasisi nyingine;

Kufuta mahakamani mashtaka yoyote ya jinai yaliyofunguliwa na mtu au taasisi nyingine katika hatua yoyote kabla hukumu kutolewa;

Kutoa maagizo kwa jeshi la polisi au vyombo chunguzi vyoyote kuchunguza taarifa yoyote ya kijinai na kutoa taarifa kwake haraka inavyowezekana;

Kuchukua hatua muhimu kwa jambo lolote lenye tija katika mashtaka ya jinai;

Kutoa miongozo inayohusu uratibu wa upelelezi na uendeshaji mashtaka;

Kuteua na kutengua mamlaka ya Waendesha Mashtaka wa umma;

Kumshauri Waziri mwenye dhamana katika masuala ya mashtaka yanayohitaji sera au hatua za kibunge;

Kuteua Maafisa Maalum ndani ya taasisi za Serikali kusimamia mali zilizozuiliwa au kutaifishwa na mahakama katika mazingira ambayo ni vigumu kuteua wasii;

Kufanya kazi nyingine ambayo zinahusiana na mashtaka ya umma;

Kuwasimamia Makatibu Sheria, Mawakili wa Serikali na watumishi wengine walioteuliwa au kuajiriwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

Kusimamia shughuli zote zinazofanywa na maafisa sheria, Mawakili wa Serikali na watumishi wengine ndani ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

Kuita afisa yoyote wa umma kutoa maelezo au taarifa kuhusiana na jambo lolote ambalo linahusu mashtaka ya umma;

Kuandaa na kuwasilisha kwa Waziri wa Katiba na Sheria taarifa ya nusu mwaka na kupeleka nakala kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; na

Kuteua au kuajiri na kuwajibisha Makatibu Sheria, Mawakili wa Serikali na watumishi wengine ndani ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.



# Majukumu ya Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka

## Bw. Joseph Sebastian Pande

Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka ndiye Msaidizi Mkuu wa Mkurugenzi wa Mashtaka na anafanya majukumu yake kadri anavyoelekezwa na Mkurugenzi wa Mashtaka. Aidha, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka ndiye Afisa Masuuli wa taasisi na anasimamia shughuli za kila siku za taasisi na anayo Mamlaka ya Nidhamu ya Watumishi kwa mujibu wa kanuni na sheria za utumishi wa umma. Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka ndiye anayeandaa kanuni za nidhamu kwa Waendesha Mashtaka na kuhakikisha viwango vya Kimataifa, Kikanda na Kimataifa vinazingatiwa. Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka ndiye anatunza kumbukumbu za Waendesha Mashtaka wa umma.



*Mkurugenzi Divisheni ya Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Tumaini Kweka akiitambulisha meza kuu na kueleza kwa ufupi juu ya Uzinduzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Vizuizi wanakoshikiliwa Watoto waliokinzana na Sheria uliofanyika jijini Dodoma.*

# Divisheni ya Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi;

**Lengo:** kutoa ushauri wa kitaalamu na huduma za uendeshaji mashtaka nchini

## MAJUKUMU

Kuratibu utekelezaji wa programu ya uendeshaji wa mashtaka;

Kuratibu na kuandaa miongozo inayohusu upelelezi na uendeshaji kesi za jinai;

Kusimamia ukaguzi, ufuatiliaji na ubora wa huduma zinazotolewa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka;

Kufuatilia na kutathimini utekelezaji wa miongozo inayotolewa na Mkurugenzi wa Mashtaka kuhusiana na upelelezi na uendeshaji mashtaka ya jinai;

Kuratibu upelelezi ili kuhakikisha ufanisi katika upelelezi unaoratibiwaa na Mwendesha Mashtaka

Kuratibu na kusimamia matumizi bora ya mwongozo wa Waendesha Mashtaka na Mwongozo wa Wapelelezi;

Kuandaa mahitaji ya mafunzo ya kisheria ili kuleta tija katika mashtaka;

Kuratibu ukaguzi wa sero za polisi na magereza;

Kuratibu ufuatiliaji wa majukumu waliyopangiwa Watumishi na Maafisa wengine ndani ya taasisi;

Kutafuta ufumbuzi wa masuala ya kisheria yanayotokana na maamuzi ya mahakama ambayo yanahitaji utekelezaji wa wadau wengine;

Kushirikisha wadau wa haki jinai katika masuala ya kesi za jinai;

Kuratibu ukusanyaji wa taarifa kutoka vyanzo mbalimbali kuhusiana na kesi zinazoendelea au kuisha ili kuleta tija katika uendeshaji wa kesi za jinai;

Kuratibu uchambuzi wa taarifa zilizokusanywa;

Kuratibu ukusanyaji taarifa za mashauri ya jinai na kuchambua kitakwimu ili kupata taarifa zitakazosaidia kuleta tija katika mashtaka na hivyo kupunguza makosa ya jinai;

Kufungua, kuendesha na kusimamia mashtaka pamoja na

Kusimamia rufaa na maombi ya jinai mahakamani kwa niaba ya Jamhuri.

*Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bi. Pendo Makondo akiwasilisha mada juu ya Kanuni, Taratibu na Miongozo inayosimamia Shughuli za Upelelezi na Uendeshaji wa Mashtaka kwenye Mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyofanyika mjini Morogoro*



# Sehemu ya Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi;

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

## MAJUKUMU

Kuratibu utekelezaji wa programu ya uendeshaji mashtaka;

Kuandaa miongozo ya uendeshaji wa mashtaka;

Kufuatilia na kutathimini utekelezaji wa miongozo inayotolewa na Mkurugenzi wa Mashtaka kuhusiana na upelelezi na uendeshaji mashtaka ya jinai;

Kuandaa na kutunza kanzi data ya Waendesha Mashtaka na Mawakili wa Serikali;

Kuratibu na kusimamia mipango na upatikanaji wa rasilimali kwa ajili ya programu ya uendeshaji mashtaka;

Kuratibu utwaaji wa uendeshaji mashtaka toka vyombo chunguzi nchini;

Kuhabarisha umma kuhusu masuala ya uendeshaji mashtaka;

Kuratibu na kushauri sera, sheria, kanuni, miongozo na viwango katika kushughulikia makosa dhidi ya binadamu na utangamano wa taifa;

Kuratibu kesi zinazohusiana na makosa dhidi ya binadamu na utangamano wa taifa;

Kuratibu utekelezaji wa sheria katika vyombo vinavyotekeleza sheria vinavyohusu makosa dhidi ya binadamu na utangamano wa taifa;

Kuratibu ushirikiano wa kitaifa, kimataifa na kikanda na wadau wengine katika mapambano dhidi ya makosa ya binadamu na utangamano wa taifa na

Kuratibu masuala yanayohusiana na mkanganyiko wa sheria za ukatili wa kijinsia na watoto.



*Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Uendeshaji wa Mashtaka kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Martenus Marandu akiwasilisha mada juu ya Taratibu za Masuala ya Kuzingatia katika Ufunguaji wa Mashtaka kwenye Mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyofanyika mjini Morogoro*

# Sehemu ya Uendeshaji wa Mashtaka

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

## MAJUKUMU

Kufuatilia, kukusanya na kuchambua taarifa za kesi zinazoendelea na zilizoisha ili kuelewa muundo na tabia za kesi;

Kukusanya na kuchambua taarifa za kesi za wakosaji wa pekee na washirika wao kwa lengo la kusimamia na kupata taarifa za kiintelejensia zitakazowezesha uendeshaji bora wa mashtaka nchini;

Kuratibu ukusanyaji taarifa za mashauri ya jinai, kuzichambua kitakwimu ili kupata taarifa zitakazosaidia kuleta tija katika uendeshaji wa mashtaka;

Kuanzisha na kutunza kanzi data ya taarifa za kiintelejensia;

Kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa za kiintelijensia na maafisa wanaoshughulikia kesi ili kuweza kuandaa mfumo wa kieletroniki wa kesi (casedocket) na uendeshaji wake mahakamani; na

Kuwezesha ubadilishanaji wa taarifa za kiintelijensia na wadau wengine ili kupunguza uhalifu na hivyo kudumisha amani na usalama wa nchi



*Washiriki wa Uzinduzi wa Taarifa ya Ukaguzi wa Vizuizi wanakoshikiliwa Watoto waliokinzana na Sheria wakifuatilia hotuba ya mgeni rasmi ambae ni Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Dkt. Khatibu Kazungu wakati akihutubia kwenye hafla fupi ya uzinduzi huo uliyofanyika Jijini Dodoma*



*Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Makosa Dhidi ya Binadamu na Utangamano wa Taifa kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Renatus Mkude akiwasilisha mada juu ya Makosa Dhidi ya Binadamu na Utangamano wa Taifa kwenye Mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyofanyika mjini Morogoro*

# Sehemu ya Makosa dhidi ya Binadamu na Utangamano wa Taifa

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

## MAJUKUMU

Kupitia na kushauri kuhusu sera, sheria, kanuni, miongozo na viwango katika kusimamia mashauri ya makosa dhidi ya binadamu na utangamano wa taifa;

Kusimamia kesi dhidi ya binadamu na utangamano wa kitaifa;

Kusimamia vyombo vinavyotekeleza sheria katika mapambano dhidi ya makosa ya binadamu na utangamano wa taifa;

Kufuatilia uanzishaji na uendeshaji wa kesi za makossa dhidi ya binadamu na utangamano wa taifa na yanayohusiana na hayo katika ngazi ya mkoa na wilaya;

Kufungua na kuendesha kesi za makosa dhidi ya binadamu na utangamano wa kitaifa na yanayohusiana nayo;

Kusimamia ufunguaji na uendeshaji wa kesi za makosa dhidi ya binadamu na utangamano wa taifa;

Kusimamia mapitio ya majalada yanayohusiana na makosa dhidi ya binadamu na utangamano wa taifa;

Kuwasiliana na mashirika ya kitaifa, kimataifa na kikanda pamoja na wadau wengine katika mapambano ya makosa dhidi ya binadamu na utangamano wa taifa;

Kusimamia chunguzi za vifo vya mashaka;

Kushauri kuhusu namna bora ya kutunza amani, usalama na utulivu wa nchi;

Kushughulikia masuala yote yanayohusu mkanganyiko wa sheria dhidi ya ukatili wa jinsia na watoto.

Kusimamia rufaa na maombi mbalimbali mahakamani yanayohusu makosa dhidi ya binadamu na utangamano wa taifa; na.

Kushughulikia rufaa na maombi mbalimbali ya kesi za makosa dhidi ya binadamu na utangamano wa taifa.



*Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu akikata utepe kuashiria Uzinduzi wa Miongozo kwa Waendesha Mashtaka na Wapelelezi katika kesi za kubaka na nyingine za kujamiiana katika hafla ya Uzinduzi huo iliyofanyika Jijini Dar es salaam.*




*Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu akikabidhi vitu mbalimbali kwa Mkuu wa Magereza Mkoa wa Rukwa Kamishna Msaidizi wa Magereza Sylvester Mrema vikiwemo Magodoro 40, mablanketi 80, sukari, Sabuni, Unga wa Uji wa lishe na nguo kwa wafungwa na Mahabusu wa Gereza la Mahabusu Sumbawanga baada ya kutembelea gereza hilo na kujionea changamoto mbalimbali zilizokuwa zinawakabili.*



*Kaimu Mkurugenzi Divisheni ya Utaifishaji Mali na Makosa yanayovuka Mipaka kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Faraja Nchimbi akichangia mada juu ya Mwongozo wa Mikataba ya kukiri Makosa ya Jinai kwenye Mafunzo ya Mwongozo kwa Wapelelezi na Waendesha Mashtaka katika kushughulikia Makosa ya Rushwa (SOPs) pamoja na Maridhiano ya Kukiri Kosa (Plea Bargaining) yaliyofanyika katika ukumbi wa St. Gaspar Jijini Dodoma*

# Divisheni ya Utaifishaji Mali, Makosa Yanayovuka Mipaka na Uhalifu Mahususi

**Lengo:** kutoa utaalamu na huduma ya kunyang'anya wahalifu au washirika wao faida zitokanazo na vitendo vya uhalifu pamoja na kuendesha kesi hizo mahakamani

## MAJUKUMU

Kuratibu utekelezaji wa sheria pamoja na masuala yote yahusuyo utaifishaji na urejeshaji mali zitokanazo na uhalifu;

Kufuatilia na kusimamia ufunguaji na uendeshaji wa kesi zinazohusiana na utaifishaji na urejeshaji wa zana zinazotumika kutenda uhalifu na mazalia yake;

Kuratibu tathmini ya ufanisi wa sheria, kanuni, miongozo na viwango kwenye masuala ya utaifishaji na urejeshaji mali zitokanazo na uhalifu na kupendekeza marekebisho yake;

Kuratibu utambuzi na ufuatiliaji wa zana zinazotumika katika kutenda uhalifu na mazalia yake;

Kuratibu ushirikiano na mashirika ya kimataifa na kikanda katika ufuatiliaji, utaifishaji na urejeshaji wa zana zinazotumika katika kutenda uhalifu na mazalia yake;

Kufuatilia na kusimamia utambuzi wa kesi zenye uwezekano wa kuwa na mali za kurejesha;

Kufuatilia na kusimamia mali zilizozuiliwa, taifishwa na kurejeshwa;

Kutoa ushauri na muongozo kuhusu maombi ya utaifishaji na urejeshaji wa mali zinazotumika katika kutenda uhalifu na mazalia yake, yanayoombwa kwa au na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

Kuratibu, kutathimini na kushauri ufanisi wa sera, sheria, kanuni, miongozo na viwango vya usimamizi wa makosa yanayovuka mipaka na kupangwa;

Kuratibu na kutoa miongozo kwa mamlaka zinazotekeleza sheria katika masuala yahusuyo makosa yanayovuka mipaka na ya kupangwa;

Kufuatilia ufunguaji na uendeshaji wa kesi za makosa yanayovuka mipaka na kupangwa katika ngazi za mikoa na wilaya;

Kufungua na kuendesha kesi za makosa yanayovuka mipaka, ya kupangwa na masuala yanayohusiana nayo;

Kusimamia mapitio ya

majalada yanayohusiana na makosa yanayovuka mipaka na ya kupangwa toka vyombo chunguzi;

Kuratibu ushirikiano na mashirika ya kitaifa, kimataifa na kikanda pamoja na wadau katika mapambano dhidi ya makosa yanayovuka mipaka na ya kupangwa;

Kuratibu na kusimamia masuala yanayohusu ubadilishanaji wa wahalifu watoro kama itakavyoelekezwa na Waziri mwenye dhamana na masuala ya sheria;

Kushauri kwenye masuala ya ushirikiano wa kesi za jinai;

Kusimamia uendeshaji wa kesi za rufaa na maombi yanayohusiana na makosa yanayovuka mipaka na ya kupangwa;

Kuwezesha uhudhuriaji wa mashahidi kutoka na kwenda nje ya nchi kutoa ushahidi;

Kuratibu na kutoa miongozo kwa mamlaka zinazotekeleza sheria katika masuala ya makosa ya kimtandao;

Kuratibu ushirikiano na mashirika ya kitaifa, kimataifa na kikanda pamoja na wadau katika mapambano dhidi ya makosa ya kimtandao; na

Kuratibu na kushauri ufanisi katika uendeshaji wa kesi za makosa ya kimtandao.



## Sehemu ya Utaifishaji na Urejeshaji Mali

*Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utaifishaji na Urejeshaji Mali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Shedrack Kimaro akiwasilisha mada juu ya Mfumo wa Kisheria wa Kimataifa na Kitaifa wa Utaifishaji Mali kwenye Mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyofanyika mjini Morogoro*

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

## MAJUKUMU

Kusimamia utekelezaji wa Sheria za utaifishaji na urejeshaji mali pamoja na masuala mengine yanayohusiana nayo;

Kutathmini na kushauri ufanisi wa Sheria, Kanuni, Miongozo na viwango kwenye masuala ya utaifishaji na urejeshaji mali zitokanazo na uhalifu na kupendekeza marekebisho yake;

Kusimamia utambuzi wa kesi zenye uwezekano wa kuwa na mali za kurejesha;

Kufungua na kuendesha kesi zinazohusu utaifishaji na urejeshaji mali ndani na nje ya nchi;

Kusimamia utambuzi na ufuatiliaji wa zana zinazotumika katika kutenda uhalifu na mazalia yake;

Kushirikiana na mashirika ya kimataifa na kikanda

katika ufuatiliaji, utaifishaji na urejeshaji wa zana zinazotumika katika kutenda uhalifu na mazalia yake;

Kusimamia utekelezaji wa sheria za utaifishaji na urejeshaji mali pamoja na masuala yanayohusiana nayo;

Kutathmini na kushauri kuhusiana na ufanisi wa sheria, Kanuni, Miongozo na viwango katika utekelezaji wa amri za utaifishaji na urejeshaji mali na kupendekeza marekebisho;

Kusimamia utekelezaji wa amri za uzuiaji na utaifishaji mali pamoja na wadau wa urejeshaji mali;

Kushirikiana na mashirika ya kimataifa na kikanda katika utekelezaji wa amri za utaifishaji na urejeshaji mali;

Kusimamia mali zilizozuiliwa, taifishwa na kurejeshwa;

Kushauri juu ya uondoshaji na ugawanyaji wa mali zilizotaifishwa;

Kuandaa na kutunza kumbukumbu za mali zote zilizo shikiliwa, zuiliwa, taifishwa na kurejeshwa; na

Kutathmini mali zilizozuiliwa, taifishwa na kurejeshwa kwa kushirikiana na taasisi nyingine za Serikali.




## Sehemu ya Makosa yanayovuka mipaka na ya kupangwa

*Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wanawake na Makundi Maalum Dkt. Dorothy Gwajima akizungumza kwenye hafla ya Uzinduzi wa Kikosi Kazi cha Ulinzi kwa Watoto dhidi ya Biashara ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu muda mfupi kabla ya kumkaribisha Mgeni rasmi Dkt. Damas Ndumbaro kuzindua rasmi Kikosi kazi hicho katika hafla iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

## MAJUKUMU

Kutathmini na kushauri kuhusiana na ufanisi wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na viwango katika usimamizi wa kesi za madawa ya kulevya, ugaidi na uharamia na kupendekeza marekebisho;

Kuwasiliana na taasisi zinazotekeleza Sheria kwenye masuala yanayohusiana na makosa ya madawa ya kulevya, ugaidi na uharamia;

Kufuatilia ufunguaji na uendeshaji wa kesi za madawa ya kulevya, ugaidi na uharamia pamoja na masuala yanayohusiana nayo katika ngazi za mikoa na wilaya;

Kufungua na kuendesha kesi za makosa ya madawa ya kulevya, ugaidi na uharamia pamoja na masuala yanayohusiana nayo.

Kusimamia na kushauri uendeshaji wa kesi za

madawa ya kulevya, ugaidi na uharamia ili kuleta tija;

Kufanya mapitio ya majalada toka vyombo chunguzi na kutoa maelekezo stahiki kuhusiana na makosa ya madawa ya kulevya, ugaidi na uharamia;

Kutoa ushauri na maoni ya kisheria kwa taasisi za kimataifa na mamlaka zinazoshughulikia makosa ya madawa ya kulevya, ugaidi na uharamia;

Kutathmini na kushauri ufanisi wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Viwango katika usimamizi wa makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu, ubadilishanaji wa wahalifu na ushirikiano katika kesi za jinai  na kupendekeza marekebisho;

Kuwasiliana na taasisi nyingine zinazotekeleza sheria katika masuala yanayohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu, ubadilishanaji wa wahalifu na ushirikiano katika kesi za jinai kulingana na Sheria na taratibu husika;

Kufungua na kuendesha kesi zinazohusiana na usafirishaji haramu wa binadamu, ubadilishanaji wa wahalifu na ushirikiano katika kesi za jinai kulingana na Sheria na taratibu husika;

Kusimamia na kushauri uendeshaji wa kesi za usafirishaji haramu wa binadamu ili kuleta tija;

Kufanya mapitio ya majalada toka vyombo chunguzi na kutoa maelekezo stahiki kuhusiana na makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu, ubadilishanaji wa wahalifu na ushirikiano katika kesi za jinai;

Kuwasiliana na taasisi za kitaifa, kimataifa na kikanda pamoja na wadau katika masuala ya usafirishaji haramu wa binadamu, ubadilishanaji wa wahalifu na ushirikiano katika kesi za jinai;

Kutoa ushauri na maoni ya kisheria kwa taasisi za kimataifa na mamlaka zinazoshughulikia makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu, ubadilishanaji wa wahalifu na ushirikiano katika kesi za jinai;

Kushughulikia na kushauri kuhusu ushirikiano katika kesi za jinai pale ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaomba au inaombwa na mamlaka za nchi nyingine;

Kushughulikia masuala yanayohusiana na wahalifu watoro, uhamishaji wa wafungwa na kutafuta mashahidi; na

Kushughulikia kesi za rufaa na maombi yanayohusiana na utwaaji wa wahalifu.



*Washiriki wa Mafunzo elekezi ambao ni waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakifuatilia mada inayowasilishwa na Kaimu Mkurugenzi Divisheni ya Utaifishaji Mali na Makosa yanayovuka Mipaka kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Faraja Nchimbi kwenye mafunzo hayo yaliyofanyika mjini Morogoro*



## Sehemu ya Makosa ya Kimtandao

*Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Makosa ya Kimtandao kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bi. Monica Mbogo akiwasilisha mada juu ya Matumizi ya TEHAMA, Makosa ya Kimtandao na Matumizi ya Mitandao ya Kijamii kwenye Mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyofanyika mjini Morogoro*

### MAJUKUMU

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

Kutathmini na kutoa ushauri kuhusiana na ufanisi wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na viwango katika usimamizi wa makosa ya kimtandao na kupendekeza marekebisho;

Kuwasiliana na taasisi zinazotekeleza sheria za makosa ya kimtandao na yale yanayohusiana nayo;

Kufuatilia ufunguaji na uendeshaji wa kesi za makosa ya kimtandao katika ngazi ya mikoa na wilaya;

Kufungua na kuendesha kesi za makosa ya kimtandao;

Kusimamia na kutoa ushauri wa uendeshaji wa kesi za makosa ya kimtandao kwa ufanisi;

Kufanya mapitio ya majalada toka vyombo chunguzi na kutoa maelekezo stahiki kuhusiana na makosa ya kimtandao;

Kuwasiliana na taasisi za kitaifa, kimataifa na kikanda pamoja na wadau katika mapambano dhidi ya makosa ya kimtandao; na

Kushughulikia kesi za rufaa na maombi yanayohusiana na makosa ya kimtandao.



*Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu akimkabidhi aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango ambaye kwa sasa ni Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania Bw. Emmanuel Tutuba Nyaraka za Mali zilizotaifishwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ambazo zimetokana na uhalifu Jijini Dodoma.*



*Picha ya pamoja ikijumuisha Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu (katikati), Balozi wa Uingereza nchini Tanzania Mhe. David Concar (wa pili kushoto), Kiongozi wa Ujumbe wa ujumbe wa Umoja wa Ulaya nchini Tanzania Balozi Manfredo Kanto (wapili kulia), Balozi wa Comoro nchini Tanzania Mhe. Ahamada El Badaovi Mohammed Farih (wakwanza kulia) wakiwa na baadhi ya Mawakili kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka waliohudhuri kwenye hafla fupi ya uzinduzi wa Mwongozo juu ya Ushirikiano wa Kimataifa kwenye Masuala ya Jinai uliofanyika Jijini Dar es salaam.*



Mkurugenzi Divisheni ya Makosa ya Rushwa, Udanganyifu, Utakatishaji fedha na Rushwa Bw. Oswald Tibabyekomya akiwasilisha mada juu ya Utayarishaji wa Nyaraka mbalimbali vikiwepo Hati za Mashtaka kwenye Mafunzo ya Upelelezi na Uendeshaji wa Kesi za Wanyamapori na Misitu yaliyodhaminiwa na Shirika lisilo la Kiserikali la PAMS Foundation mjini Morogoro.

# DIVISHENI YA MAKOSA YA UDANGANYIFU, UTAKATISHAJI FEDHA NA RUSHWA

**Lengo:** kutoa utaalamu na huduma ya mashtaka kwa makosa ya udanganyifu, utakatishaji fedha, rushwa, mazingira na maliasili

## MAJUKUMU

Kupitia na kutoa ushauri kwenye sera, Sheria, kanuni, miongozo na viwango katika usimamizi wa makosa ya udanganyifu, utakatishaji fedha na rushwa;

Kuratibu kesi za rushwa katika mahakama kuu kitengo cha makosa ya rushwa na uhujumu uchumi na mahakama za chini;

Kuratibu taasisi zinazotekeleza sheria katika makosa ya udanganyifu, utakatishaji fedha, rushwa na masuala yanayohusiana nayo;

Kusimamia ufunguaji na uendeshaji wa kesi za udanganyifu na rushwa katika ngazi za mikoa na wilaya;

Kufungua na kuendesha kesi za rushwa na udanganyifu;

Kusimamia mapitio ya majalada ya kesi za utakatishaji fedha, rushwa na udanganyifu;

Kuratibu ushirikiano na mashirika ya kitaifa, kimataifa na kikanda pamoja na wadau katika kupambana na makosa ya udanganyifu, utakatishaji fedha na rushwa;

Kusimamia kesi za rufaa na maombi yanayohusiana na makosa ya udanganyifu, utakatishaji fedha na rushwa; na

Kushughulikia kesi za rufaa na maombi yanayohusiana na rushwa na udanganyifu.



Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu akikata utepe kuashiria Uzinduzi wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Wadau katika Upelelezi wa Utakatishaji Fedha Haramu, Ugaidi na Ufadhili wa Ugaidi Jijini Dodoma.




Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Bw. Sylvester Mwakitalu akikabidhi nakala za Mwongozo wa Ushirikiano wa Wadau katika Upelelezi wa Utakatishaji Fedha Haramu, Ugaidi na Ufadhili wa Ugaidi kwa Bw. Oswald Tibabyekomya mara baada ya kuzindua mwongozo huo Jijini Dodoma.

*Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Udanganyifu na Utakatishaji Fedha kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Seth Mkemwa akiwasilisha mada juu ya Mwongozo wa Mikataba ya Kukiri Makosa ya Jinai kwenye Mafunzo juu ya Mwongozo kwa Wapelelezi na Waendesha Mashtaka katika kushughulikia Makosa ya Rushwa (SOPs) pamoja na Maridhiano ya Kukiri Kosa (Plea Bargaining) yanayofanyika katika ukumbi wa St. Gaspar Jijini Dodoma*



# Sehemu ya makosa ya udanganyifu na utakatishaji fedha

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

## MAJUKUMU

Kutathmini na kushauri kuhusiana na ufanisi wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na viwango katika usimamizi wa kesi za udanganyifu na utakatishaji fedha na kupendekeza maboresho;

Kuwasiliana na taasisi zinazotekeleza sheria katika masuala yanayohusiana na makosa ya udanganyifu na utakatishaji fedha na yanayohusiana nayo;

Kufuatilia ufunguaji na uendeshaji wa kesi za makosa ya udanganyifu na utakatishaji fedha katika ngazi za mikoa na wilaya;

Kufungua na kuendesha kesi zinazohusiana na makosa ya rushwa na udanganyifu;

Kusimamia na kushauri uendeshaji wa kesi za makosa ya udanganyifu na utakatishaji fedha ili kuleta tija;

Kufanya mapitio ya majalada kutoka vyombo chunguzi na kutoa maelekezo stahiki kuhusiana na makosa ya udanganyifu na utakatishaji fedha;

Kuratibu ushirikiano na mashirika ya kitaifa, kimataifa na kikanda pamoja na wadau katika mapambano dhidi ya makosa ya udanganyifu na utakatishaji fedha; na

Kushughulikia kesi za rufaa na maombi yanayohusiana na makosa ya udanganyifu na utakatishaji fedha.



## Sehemu ya Makosa ya Rushwa

*Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Makosa ya Rushwa kutoka Ofisi kya Taifa ya Mashtaka Bw. Zakaria Ndaskoi akiwasilisha mada juu ya ushughulikiwaji wa kesi za Rushwa katika taarifa ya mwezi Mei, 2022 wakati wa kikao cha Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa na Menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kilichofanyika Jijini Dodoma.*

## MAJUKUMU

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

Kutathmini na kushauri kuhusiana na ufanisi wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na viwango katika usimamizi wa kesi za rushwa na kupendekeza maboresho;

Kuwasiliana na taasisi zinazotekeleza sheria za makosa ya rushwa na yanayohusiana nayo;

Kusimamia ufunguaji na uendeshaji wa kesi za rushwa na yanayohusiana nayo katika ngazi ya mkoa na wilaya;

Kufungua na kuendesha kesi za rushwa na masuala yanayohusiana nayo;

Kusimamia na kushauri njia bora za uendeshaji wa kesi za rushwa;

Kufanya mapitio ya majalada kutoka vyombo chunguzi na kutoa maelekezo stahiki kuhusiana makosa ya rushwa;

Kuratibu ushirikiano na mashirika ya kitaifa, kimataifa na kikanda pamoja na wadau katika mapambano dhidi ya rushwa; na

Kushughulikia rufaa na maombi ya kesi za rushwa.



## Sehemu ya Makosa ya Mazingira na Maliasili

*Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Makosa dhidi ya Mazingira na Maliasili kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bi. Rosemary Shio akiwasilisha mada juu ya Masuala ya Msingi ya kuzingatia katika vikao vya awali na baada ya ukamataji wa mshtakiwa wakati wa Mafunzo ya Upelelezi na Uendeshaji wa Kesi za Wanyamapori na misitu kwa Wakuu wa Upelelezi na Waendesha Mashtaka nchini yaliyofanyika mjini Moshi.*

## MAJUKUMU

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

Kuutathmini na kushauri kuhusiana na ufanisi wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na viwango katika usimamizi wa kesi za mazingira na mali asili na kupendekeza maboresho;

Kuwasiliana na taasisi zinazotekeleza sheria za makosa ya mazingira na mali asili;

Kusimamia ufunguaji na uendeshaji wa kesi za mali asili na mazingira;

Kusimamia na kufuatilia kesi za mazingira na mali asili zinazoendeshwa na taasisi nyingine;

Kusimamia mapitio ya majalada ya kesi za mazingira na mali asili kutoka vyombo chunguzi;

Kuratibu ushirikiano na mashirika ya kimataifa na kikanda pamoja na wadau katika mapambano dhidi ya makosa ya mazingira na mali asili; na

Kushughulikia rufaa na maombi ya kesi za mali asili na mazingira




*Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Bw. Sylvester Mwakitalu (aliyekaa wanne kutoka kulia) akiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa Uzinduzi wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Wadau katika Upelelezi wa Utakatishaji Fedha Haramu, Ugaidi na Ufadhili wa Ugaidi uliofanyika Jijini Dodoma.*




*Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro akihutubia kwenye hafla ya Uzinduzi wa Mwongozo wa Ushirikiano wa Wadau katika Upelelezi wa Utakatishaji Fedha Haramu, Ugaidi na Ufadhili wa Ugaidi iliyofanyika Jijini Dodoma.*



# Divisheni ya Usimamizi wa Kesi na Uratibu wa Upelelezi

*Mkurugenzi Idara ya Usimamizi wa Kesi na Uratibu wa Upelelezi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bi. Neema Mwanda akiwasilisha mada juu ya Regista za Kutunza Kumbukumbu za Kesi kwenye Mafunzo ya Mwongozo kwa Wapelelezi na Waendesha Mashtaka katika kushughulikia Makosa ya Rushwa (SOPs) pamoja na Maridhiano ya Kukiri Kosa (Plea Bargaining) yanayofanyika katika ukumbi wa St. Gaspar Jijini Dodoma*

**Lengo:** kutoa utaalamu katika usimamizi wa kesi na uratibu wa upelelezi

## MAJUKUMU

Kutoa maelekezo katika usimamizi, ukaguzi na ufuatiliaji wa ubora katika uendeshaji wa huduma zinazotolewa na Ofisi;

Kusimamia mahitaji ya mafunzo katika masuala ya sheria kwa vitendo pamoja na usimamizi wa taarifa ili kuhakikisha ufanisi katika uendeshaji kesi;

Kusimamia utendaji kazi wa kila Mwendesha Mashtaka, majukumu ya Jukwaa la Taifa la Haki Jinai, Kamati za kusimamia kesi na kuandaa ripoti na kuiwasilisha kwa Mkurugenzi wa Mashtaka;

Kutekeleza mpango wa ulinzi kwa mashahidi;

Kusimamia maandalizi ya miongozo inayohusiana na uendeshaji wa kesi za jinai na utekelezaji wa maelekezo ya jumla ya upelelezi;

Kusimamia utekelezaji wa maagizo yanayotolewa na Mkurugenzi wa Mashtaka kuhusiana na upelelezi wa kesi za jinai ili kuleta ufanisi;

Kusimamia uratibu wa upelelezi ili kuhakikisha ufanisi katika upelelezi unaoratibiwa na Mwendesha Mashtaka;

Kusimamia na kufanya kaguzi katika maeneo ambayo mahabusu wanahifadhiwa na kuchukua hatua stahiki;

Kufanya kazi na wadau wengine wa Haki Jinai ili kuwezesha uratibu wa kesi na ubadilishanaji wa taarifa; na

Kuanzisha na kutunza mahusiano kati ya Ofisi, vyombo chunguzi na ushirikiano wa kitaifa na kimataifa.

*Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Usimamizi wa Kesi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bi. Javelin Rugaihuruza akitoka neno la kumkaribisha Mkurugenzi Idara ya Usimamizi wa Kesi na Uratibu wa Upelelezi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bi. Neema Mwanda (hayupo pichani) kufungua mafunzo kuhusu Utumiaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika masuala ya kesi kwa Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa na Wilaya pamoja na Waendesha Mashtaka Viongozi yaliyofanyika Jijini Dar es Salaam.*



# Sehemu ya Usimamizi wa Kesi

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

## MAJUKUMU

Kukagua na kufuatilia ubora juu ya huduma za uendeshaji kesi;

Kutathmini uhitaji wa mafunzo ya uendeshaji wa masuala ya sheria kwa vitendo na kuhakikisha ufanisi katika uendeshaji wa kesi;

Kuanzisha na kutunza orodha itakayosaidia kumbukumbu na ugatuzi wa kazi;

Kutathmini taarifa za kesi kulingana na miongozo na viwango vya taasisi;

Kubaini masuala muhimu yanayojitokeza kwenye kesi zinazoamuliwa na kufanya uratibu na wadau wengine na kutoa mapendekezo;

Kutathmini utendaji kazi wa kila Mwendesha Mashtaka na kutoa mapendekezo;

Kuwezesha majukumu ya jukwaa la haki jinai;

Kuwezesha kamati za kusimamia kesi kwenye ngazi za wilaya, mkoa na kitaifa pamoja na majukwaa mengine;

Kutunza kanzidata na mfumo wa taarifa;

Kuanzisha na kutekeleza mpango wa ulinzi wa mashahidi;

Kusajili na kutunza rejesta ya kesi zinazosajiliwa na au dhidi ya jamhuri;

Kurekodi kesi zilizosajiliwa mahakamani;

Kuwasilisha nyaraka zinazohusiana na kesi za jamhuri;

Kutunza majalada ya kesi zinazoihusu jamhuri;

Kuandaa na kutunza rejesta ya mawasiliano toka kwa umma katika kesi za jamhuri na zile zilizofunguliwa dhidi ya jamhuri; na

Kupeleka nyaraka na mawasiliano mengine yanayohusiana na kesi



*Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Uratibu wa Upelelezi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Peter Mauggo akiwasilisha mada juu ya Kanuni za Malipo ya Mashahidi kwenye Kikao kazi cha Wakuu wa Mashtaka Mikoa na Menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Jijini Dodoma*

# Sehemu ya Uratibu wa Upelelezi

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

## MAJUKUMU

Kuandaa miongozo inayohusiana upelelezi wa kesi za jinai;

Kufuatilia na kutathmini utekelezaji wa miongozo inayotolewa na mkurugenzi wa mashtaka kuhusiana na upelelezi wa kesi za jinai;

Kuratibu upelelezi ili kuhakikisha ufanisi katika upelelezi unaoratibiwa na Mwendesha Mashtaka;

Kufanya ufuatiliaji juu ya utekelezaji wa maelekezo ya jumla ya upelelezi ili kuleta ufanisi;

Kusimamia na kufanya kaguzi katika maeneo ambayo mahabusu wanahifadhiwa na kuchukua hatua stahiki;

Kufanya kazi na wadau wengine wa haki jinai ili kuwezesha uratibu wa kesi na ubadilishanaji wa taarifa;

Kuwezesha majukumu ya jukwaa la haki jinai;

Kuwasiliana na ofisi za taifa za mashtaka wilayani na mikoani kwa lengo la kuratibu upelelezi;

Kuandaa na kusambaza miongozo kuhusu upelelezi na kusimamia upelelezi wa kesi za jinai;

Kukagua na kufatilia ubora wa huduma zinazotolewa na divisheni;

Kutoa mapendekezo kuhusu utendaji kazi wa kila Mwendesha Mashtaka;

Kuratibu uendelezaji wa ujuzi kuhusu masuala ya kisheria ili kuhakikisha ufanisi katika upelelezi unaoongozwa na Mwendesha Mashtaka; na

Kuanzisha na kudumisha mahusiano kati ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, vyombo chunguzi na mashirika mengine ya kitaifa na kimataifa




*Picha ya pamoja ikijumuisha Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu (wapili kulia), akiwa na baadhi ya watumishi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Makao Makuu Jijini Dodoma na Mkoa wa Shinyanga, pamoja na Jeshi la Magereza na Polisi walipotembelea gereza la Wilaya ya Shinyanga walipokuwa kwenye ziara ya kutembelea Magereza nchini.*



*Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu akisalimiana na Askari Magereza wa Gereza Kuu Uyui Mkoani Tabora kabla ya kuingia gerezani kusikiliza changamoto mbalimbali zinaziwakabili Wafungwa na Mahabusu.*



*Washiriki wa Kikao kazi baina ya Menejimenti, Wakuu wa Mashtaka Mikoa, Wilaya na Waendesha Mashtaka Viongozi wakifuatilia kwa umakini mada mbalimbali zinazowasilishwa kwenye kikao kazi hicho  kilichofanyika Jijini Dodoma.*



## Divisheni ya Utawala na Raslimali Watu

*Mkurugenzi wa Utawala na Raslimali Watu kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Titus Mkapa akitoa utambulisho kwa washiriki wa Mafunzo elekezi ya awali kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyofanyika mjini Morogoro*

**Lengo:** Kutoa utaalamu na huduma za kiutawala na usimamizi wa rasilimali watu katika Ofisi. Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi

# MAJUKUMU

Kutoa mikakati kwa menejimenti juu ya uendeshaji wa masuala ya Rasilimali watu ikujumuisha masuala ya ajira, uendelezaji wa rasilimali watu, upandishwaji wa vyeo, kutoa motisha, kuweka vivutio vya kazi kwa watumishi ili waendelee kuwepo kwenye Tasisi, kutoa motisha na kudhibiti viwango vya kazi;

Kuandaa mafao ya mstaafu na likizo kwa watumishi;

Kuhakikisha uwepo wa tija na ufanisi katika usimamizi na Matumizi ya Raslimaliwatu katika ofisi;

Kuwa kiungo kati ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na Ofisi ya Rais Menejimenti ya utumishi wa Umma na utawala bora katika usimamiaji wa Sera na sheria za ajira zinazohusu utumishi wa umma;

Kutoa takwimu za kiutumishi na kuzihuisha; na

Kukusanya, kuchambua, kuweka na kusambaza takwimu na taarifa zinazohusiana na mipango ya uendelezaji Raslimaliwatu.



## Sehemu ya Utawala

*Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala Bw. Leonard Mehta akiwasilisha mada juu ya Maadili katika Utumishi wa Umma wakati wa Mafunzo ya Upelelezi na Uendeshaji wa Kesi za Wanyamapori na Misitu kwa Wakuu wa Upelelezi na Waendesha Mashtaka nchini yaliyofanyika mjini Moshi*

# MAJUKUMU

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

Kutafsiri na kuhakikisha Sheria, Kanuni za kudumu, machapisho na sheria za kazi zinazohusu utawala na usimamizi wa Raslimaliwatu zinafuatwa;

Kudumisha mahusiano ya watumishi na maslahi yao ikiwemo afya, usalama, michezo na tamaduni;

Kutoa huduma za masjala, kumbukumbu za ofisi, huduma za mawasiliano, na utumaji wa nyaraka;

Kushughulikia masuala ya protokali;

Kuwezesha huduma za utoaji wa ulinzi, usafiri na mahitaji ya kila siku;

Kuwezesha huduma za uhifadhi ikiwemo matengenezo ya vifaa vya ofisi, majengo na mazingira;

Kuratibu utekelezaji na ukuzaji wa maadili na masuala muhimu katika utumishi wa umma;

Kutekeleza masuala ya mtambuka ikiwemo jinsia, ulemavu, ukimwi na magonjwa yasiyoambukizwa na masuala ya mazingira;

Kuratibu utekelezaji wa uboreshaji wa mifumo ya utendaji kazi;

Kushauri juu ufanisi wa utendaji wa ofisi;

Kuratibu maandalizi/ utekelezaji wa mkataba wa huduma kwa wateja; na

Kuratibu utekelezaji wa ushirikishwaji wa sekta binafsi.



## Sehemu ya Usimamizi wa Raslimali Watu

*Picha ya pamoja ikijumuisha Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro (aliyekaa katikati), Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Bw.Joseph Pande (kulia), Mkurugenzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania Dkt. Hamisi Amani (kushoto) wakiwa katika picha ya pamoja na washiriki wa Mafunzo elekezi ya awali kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyofanyika mjini Morogoro.*

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

## MAJUKUMU

Kuratibu masuala ya ajira, kupangia vituo vya kazi, kuthibitishwa kazini, kupandishwa vyeo na uhamisho kwa watumishi;

Kuwezesha mafunzo na ukuaji wa maendeleo ya kazi (maendeleo ya kitaaluma, kukuza ujuzi, kukuza utendaji wa kazi na maandalizi ya kustaafu);

Kuratibu mafunzo kazi kwa ajili ya waajiriwa wapya katika utumishi wa umma;

Kuandaa na kutekeleza mipango ya Rasilimali Watu na maendeleo;

Kusimamia mishahara na malipo;

Kuandaa na kuboresha kumbukumbu za watumishi ikiwa ni pamoja na likizo za mwaka, kustaafu, ugonjwa, uzazi na masomo;

Kuandaa maslahi na stahili za watumishi;

Kuratibu utekelezaji wa upimaji kazi wa wazi kwa watumishi;

Kuandaa makisio ya ikama ya watumishi na bajeti kwa kila mwaka;

Kuandaa na kuwezesha utekelezaji wa mpango wa kurithishana madaraka; na

Kuanzisha na kuratibu mafunzo ya ndani na ya kazi kwa watumishi;



## Divisheni ya Mipango

*Mkurugenzi wa Idara ya Mipango kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Makao Makuu Jijini Dodoma Bw. Mussa Magunguli akitoa Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na changamoto zilizojitokeza pamoja na Taarifa ya Makadilio ya Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa mwaka wa fedha 2023/2024 mjini Morogoro*

## MAJUKUMU

**Lengo:** Kutoa utaalamu katika maeneo ya mipango, utekelezaji wa bajeti, ufuatiliaji na tathmini

Kuratibu maandalizi na utekelezaji wa mipango na bajeti;

Kuratibu maandalizi ya michango kwenye hotuba ya bajeti ya Waziri na ripoti ya kila mwaka ya uchumi;

Kuratibu maandalizi, utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya mipango ya maendeleo;

Kuratibu maandalizi na utekelezaji wa miradi, programu za maendeleo na ukusanyaji wa rasimali zinazohitajika;

Kuandaa, kutekeleza na kuboresha mpango wa usimamizi wa vihatarishi;

Kuandaa rejesta ya vihatarishi; na

Kutoa mwongozo na ushauri ili kuhakikisha kuwa vihatarishi vinatambuliwa, tathminiwa na kupunguzwa.



## Sehemu ya Mipango na Bajeti

*Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Mipango na Bajeti Bw. Oswald Kyamani kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Makao Makuu Jijini Dodoma akitoa maelekezo kwa Maafisa Bajeti juu ya Kikao kazi cha Uandaaji wa Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu Nusu Mwaka 2022/2023 (Progressive Report), Re-allocation na Maoteo ya Bajeti 2022/2023 kilichofanyika Jijini Arusha*

## MAJUKUMU

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

Kuratibu masuala ya ajira, kupangia vituo vya kazi, kuthibitishwa kazini, kupandishwa vyeo na uhamisho kwa watumishi;

Kuratibu uandaaji wa mpango kazi wa mwaka, kati na mpango mkakati;

Kuainisha miradi, programu, mipango kazi na kuendeleza mikakati ya ukusanyaji wa rasilimali;

Kushirikiana na wizara ya Katiba na Sheria, Wizara ya Fedha na Uchumi katika uandaaji wa mpango mkakati na bajeti;

Kutoa msaada wa kiufundi katika mchakato wa kuandaa mpango mkakati na bajeti; na

Kuandaa maandiko na makubaliano ya miradi na programu kwa ajili ya kupata rasilimali fedha za ndani na nje ya nchi;



## Sehemu ya Ufuatiliaji na Tathimini

*Mkurugenzi Msaidizi wa Ufuatiliaji na Tathimini*

***Bw. Yohana Ngao***

## MAJUKUMU

**Sehemu hii inaongozwa na Mkurugenzi Msaidizi**

Kufuatilia utekelezaji mpango kazi wa mwaka na mpango mkakati;

Kuandaa ripoti za utekelezaji;

Kuandaa ripoti ya uendeshaji mashtaka nchini;

Kutoa michango katika maandalizi ya mipango ya kitaifa, programu na masuala ya kibajeti ikiwemo uanishaji wa malengo na viashiria vya utendaji;

Kutoa misaada ya kiufundi katika kusimika mifumo ya tathimini na ufuatiliaji;

Kufanya utafiti na tathmini juu ya matokeo za mipango, miradi na programu;

Kukusanya maoni ya wadau kuhusiana na huduma zinazotolewa;

Kuratibu utekelezaji wa mwaka na nusu mwaka;

Kuandaa, kutekeleza na kuhuisha mpango wa usimamizi wa vihatarishi;

Kuandaa na kusimamia rejesta ya vihatarishi; na

Kutoa mwongozo na ushauri ili kuhakikisha kuwa vihatarishi vinatambuliwa, tathminiwa na kupunguzwa



*Picha ya pamoja ikijumuisha Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Arusha Bw. Abdallah Chavula (aliyekaa katikati) akiwa na washiriki wa Kikao kazi cha Uandaaji wa Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu Nusu Mwaka 2022/2023 (Progressive Report), uhamisho wa Vifungu vya Bajeti na Maoteo ya Bajeti 2022/2023 kilichofanyika Jijini Arusha*



*Baadhi ya washiriki wa kikao kazi cha Uandaaji wa Taarifa ya Utekelezaji wa Majukumu Nusu Mwaka 2022/2023 (Progressive Report), uhamisho wa Vifungu vya Bajeti na Maoteo ya Bajeti 2022/2023 wakifuatilia kwa umakini hotuba ya Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Joseph Pande wakati akihutubia kwenye kikao kazi hicho kilichofanyika Jijini Arusha*



## Kitengo cha Ununuzi na Ugavi

*Mkurugenzi wa Manunuzi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Jimmy Ntimaza akiwasilisha mada juu ya Taratibu za Manunuzi na Ugavi kwenye Kikao kazi cha Wakuu wa Mashtaka Mikoa na Menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kilichofanyika Jijini Dodoma*

**Lengo:** Kutoa utaalamu na huduma za ununuzi na ugavi

# MAJUKUMU

Kushauri juu ya ununuzi, usimamizi wa vifaa na usambazaji wake;

Kufuatilia na kuhakikisha michakato ya ununuzi na taratibu zake zinafuatwa kwa mujibu wa sheria ya ununuzi wa umma;

Kuandaa mpango wa ununuzi wa mwaka;

Kununua, kutunza na kusimamia ugavi kulingana na mahitaji;

Kutunza na kusimamia usambazaji wa vifaa vya ofisi;

Kutunza na kuhuisha kumbukumbu za ununuzi na ugavi;

Kutoa huduma za sekretarieti kwa bodi ya zabuni;

Kuweka vigezo / viwango na kufuatilia uhalisia wa thamani ya bidhaa na huduma zinazonunuliwa; na

Kuandaaa mpango kazi, taarifa ya utekelezaji na bajeti ya ununuzi ya kitengo





*Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo akiwa ameongozana na Viongozi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakiwa katika ziara ya kutembelea Mradi wa Ujenzi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoa wa Morogoro kwa lengo la kujionea hali halisi ya maendeleo ya ujenzi.*



*Menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa, Wahasibu na Makatibu Sheria wakiongozwa na Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu na Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Joseph Pande wakitembelea ujenzi wa jengo jipya la Makao Makuu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ambalo linaendelea kujengwa maeneo ya Njedengwa Jijini Dodoma.*



## Kitengo cha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)

*Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Frank Shame akiwasilisha mada juu ya Majukumu ya Kitengo cha TEHAMA na Matumizi ya Barua Pepe Serikalini kwenye Mafunzo elekezi ya awali kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyofanyika mjini Morogoro.*

**Lengo:** Kutoa utaalamu na huduma kwa matumizi ya TEHAMA

# MAJUKUMU

Kutekeleza mpango mkakati wa TEHAMA na Serikali Mtandao;

Kuendeleza na kuratibu mifumo TEHAMA kwa kushirikiana na Wakala wa Serikali Mtandao;

Kuhakikisha kwamba vifaa na programu za TEHAMA zinasimamiwa na kutunzwa

Kuratibu na kutoa msaada katika ununuzi wa programu na vifaa vya TEHAMA;

Kuanzisha na kuratibu matumizi ya mawasiliano ya barua pepe na mitandao;

Kufuatilia na kusimamia usalama wa mifumo ya mawasiliano na taarifa; na

Kufanya tafiti na kushauri juu ya matumizi ya TEHAMA kama chombo cha kuboresha utoaji wa huduma.




*Maafisa TEHAMA kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakitoa usaidizi wa kiufundi kwa washiriki wa Mafunzo ya Utumiaji wa Mfumo wa Kielektroniki wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika masuala ya kesi kwa Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa na Wilaya pamoja na Waendesha Mashtaka Viongozi yaliyofanyika Jijini Dar es salaam*



*Picha ya pamoja ikijumuisha Mkurugenzi Divisheni ya Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Makao Makuu Jijini Dodoma Bw. Tumaini Kweka (aliyekaa katikati), Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Uratibu wa Upelelezi Bw. Peter Maugo (aliyekaa wapili kushoto), Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Frank Shame (wa pili kulia), wakiwa na baadhi ya Makatibu Sheria na Mawakili wa Serikali walioshiriki katika Mafunzo ya Utumiaji wa Mfumo wa Kielekitroniki wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika masuala ya Kesi kwa Makatibu Sheria na baadhi ya Mawakili wa Serikali wanaoshughulika na Takwimu yaliyofanyika Jijini Dar es salaam.*



## Kitengo cha Uhasibu na Fedha

*Mhasibu Mkuu kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashkata Bw. Mourice Ngaka akiwasilisha Taarifa ya Fedha za Malipo ya Mashahidi kwenye Kikao kazi kilichohusisha Menejimenti, Wakuu wa Mashtaka Mikoa na Wilaya na Waendesha Mashtaka Viongozi kilichofanyika Jijini Dodoma.*

**Lengo:** Kutoa huduma za usimamizi wa kifedha na utunzaji wa vitabu vya vitabu vya kihasibu

## MAJUKUMU

Kuandaa malipo ya mishahara ikiwemo makato yaliyoainishwa kisheria;

Usimamizi wa mishahara;

Kuandaa taarifa za pensheni;

Kutunza kumbukumbu;

Kuwasilisha orodha ya malipo hazina;

Kuweka fedha na kuwasilisha hundi benki;

Kuandaa ripoti ya kila mwezi;

Kulipa fedha/hundi kwa wafanyakazi na wateja (watoa huduma);

Kulipa malipo ya jumla;

Kutunza vitabu vya fedha;

Kurekodi na kuhakiki masurufu yaliyotolewa;

Kuandaa na kufanya malipo;

Kusimamia mapato kulingana na kanuni na miongozo;

Kukusanya kodi ya kila mwaka, ada za maombi na vyanzo vingine;

Kusimamia na kukusanya mapato; na

Usuluhishi wa kibenki.

Kuandaa nyaraka za pensheni;

Kutunza kumbukumbu za pensheni;

Usimamizi wa bajeti;

Kufuatilia ugawaji na matumizi ya fedha;

Kuandaa taarifa za mwisho na taarifa nyingine za kifedha;

Kuhakiki na kupitisha nyaraka za malipo kwa mujibu wa kanuni;

Kuhakiki nyaraka za kifedha kwa mujibu sheria, kanuni na miongozo inayosimamia fedha za umma; na

Kutoa majibu kwa hoja za ukaguzi.



*Baadhi ya washiriki wa kikao kazi cha Wahasibu na Makatibu Sheria wanaofanya shughuli za kihasibu katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakifuatilia mada mbalimbali zilizowasilishwa katika kikao kazi hicho kilichofanyika Jijini Dodoma.*



*Washiriki wa kikao kazi cha Wakuu wa Mashtaka Mikoa, Wahasibu na Makatibu Sheria wanaofanya shughuli za kihasibu katika Mikoa na Menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakifuatilia mada iliyowasilishwa na Mhasibu Mkuu kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Mourice Ngaka katika kikao kilichofanyika Jijini Dodoma.*



## Kitengo cha Masjala ya Sheria

*Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Masjala ya Sheria kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bi. Agnes Mtindi akiwasilisha mada juu ya Majukumu ya Kitengo cha Masjala ya Sheria, Kazi za Makatibu Sheria na Aina mbalimbali za Rejesta kwenye Mafunzo elekezi ya awali kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyofanyika mjini Morogoro.*

**Lengo:** Kutoa huduma za masjala katika Ofisi ya Taifa ya Mashtaka

## MAJUKUMU

Kusajili na kutunza rejesta ya kesi zote zilizofunguliwa mahakamani na zina zoshughulikiwa na mkurugenzi wa mashtaka;

Kupeleka nyaraka zinahusiana na kesi zinazomuhusu mkurugenzi wa mashtaka;

Kutunza majalada ya kesi zinazoshughulikiwa na mkurugenzi wa mashtaka; na

Kupokea na kutuma majalada ya kesi kutoka na kwenda kwa taasisi uchunguzi.



*Baadhi ya washiriki wa kikao kazi cha Mkurugenzi wa Mashtaka na Makatibu Sheria wakimsikiliza Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala Bw. Leonard Mehta (hayupo pichani) wakati akitoa neno la kuhitimisha kikao kazi hicho kilichofanyika Jijini Dodoma.*



*Baadhi ya washiriki wa kikao kazi cha Mkurugenzi wa Mashtaka na Makatibu Sheria wakimsikiliza Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala Bw. Leonard Mehta (hayupo pichani) wakati akitoa neno la kuhitimisha kikao kazi hicho kilichofanyika Jijini Dodoma.*




*Mkuguzi Mkuu wa Ndani kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka CPA. Idd Mboweto akiwasilisha mada juu ya Usimamizi wa Mali zilizotaifishwa kutokana na uhalifu kwenye Mafunzo ya Upelelezi na Uendeshaji wa Kesi za Wanyamapori na misitu kwa Wakuu wa Upelelezi na Waendesha Mashtaka nchini yaliyofanyika mjini Moshi*

## Kitengo cha Ukaguzi wa Ndani

**Lengo:** Kutoa huduma za ushauri kwa Afisa wa Masuuli katika usimamizi sahihi wa rasilimali

# MAJUKUMU

Kufanya mapitio na kutoa ripoti kuhusu udhibiti katika upokeaji, utunzaji na matumizi ya rasilimali fedha;

Kufanya mapitio na kutoa ripoti juu ya uzingatiaji wa taratibu uendeshaji na kifedha kwa mujibu wa sheria, kanuni na maelekezo kwa ajili ya udhibiti wa matumizi;

Kufanya mapitio na kutoa ripoti juu ya usahihi wa uainishaji na ugawaji wa mapato na matumizi;

Kuandaa taratibu za ukaguzi ambazo hazikizani na viwango vya kimataifa;

Kufanya mapitio na kutoa ripoti juu ya usahihi, uadilifu wa shughuli za kifedha, taarifa, kuandaa taarifa za kifedha na taarifa nyingine;

Kufanya mapitio na kutoa ripoti juu ya mfumo unaotumika kulinda mali na kuthibitisha uwepo wake;

Kufanya mapitio na kutoa ripoti juu ya uendeshaji au programu ili kuona kama matokeo yanaendana na madhumuni na malengo yaliyowekwa.

Kufanya mapitio na kutoa ripoti juu ya majibu yaliyotolewa na menejimenti kuhusu ripoti za ukaguzi wa ndani, na kusaidia menejimenti katika utekelezaji wa mapendekezo ya ripoti na ufuatiliaji juu ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na mdhibiti na mkaguzi mkuu wa hesabu za Serikali;

Kufanya mapitio na kutoa ripoti juu ya utoshelevu wa udhibiti katika mifumo ya kompyuta.

Kuandaa na kutekeleza mpango mkakati wa ukaguzi; na

Kufanya ukaguzi wa utendaji juu ya tathmini ya miradi ya maendeleo





*Baadhi ya washiriki wa Mafunzo ya Upelelezi na Uendeshaji wa Kesi za Wanyamapori na Misitu kwa Wakuu wa Upelelezi na Waendesha Mashtaka nchini wakifuatilia mada iliyowasilishwa na Mkaguzi Mkuu wa Ndani kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka CPA. Idd Mboweto kwenye mafunzo hayo yaliyofanyika mjini Morogoro.*



## Kitengo cha Huduma za Utafiti na Maktaba

*Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Maktaba ya Sheria na Utafiti Bi. Lilian Nyenza akiwasilisha mada juu ya Majukumu ya Kitengo cha Maktaba ya Sheria na Utafiti kwenye Mafunzo elekezi ya awali kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyofanyika mjini Morogoro.*

**Lengo:** Kutoa utaalamu na huduma katika utafiti wa kisheria, huduma za uchapishaji na maktaba

# MAJUKUMU

Kuufanya utafiti wa kisheria katika uendeshaji wa mashtaka na masuala yanayohusiana nayo;

Kuwajulisha watumiaji wa maktaba kuhusu bidhaa mpya za sheria;

Kuwekea maktaba vifaa vya kutosha vya utafiti, nyenzo na nyaraka za rejea;

Kuweka katika maktaba katiba, sheria na nyaraka mbali mbali za kisheria;

Kutunza vitabu vya rejea vya kesi, machapisho na majarida ya kisheria na magazeti;

Kutunza rejesta ya machapisho ya rejea;

Kuwezesha uazimaji wa machapisho ya rejea;

Kuanzisha mfumo wa ubadilishanaji wa sheria zinazohusiana na uendeshaji wa mashtaka na kazi kutoka nchi zilizo katika jumuiya ya madola na zisizo za jumuiya; na

Kushauri juu ya ununuzi wa machapisho ya kisheria.



*Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Huduma za Utafiti na Maktaba Bi. Lilian Nyenza akiwa katika Maktaba ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Makao Makuu jijini Dodoma.*



*Waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakimsikiliza kwa umakini Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Maktaba ya Sheria na Utafiti Bi. Lilian Nyenza wakati akiwasilisha mada kwenye mafunzo elekezi kwa waajiriwa wapya yaliyofanyika mjini Morogoro.*



# Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

*Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini Bi. Rebecca Kwandu akiwasilisha mada juu ya Majukumu ya Kitengo cha Mawasiliano Serikalini kwenye Mafunzo elekezi ya awali kwa waajiriwa wapya wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka yaliyofanyika mjini Morogoro.*

**Lengo:** Kutoa utaalamu na huduma za habari, mawasiliano, mazungumzo na umma pamoja na vyombo vya habari

## MAJUKUMU

Kupata na kusambaza taarifa kwaajili ya kuhabarisha umma juu ya sera, programu kazi na maboresho yanayofanyika;

Kuratibu utoaji wa taarifa kwenye vyombo habari;

Kufanya mazungumzo na umma pamoja na vyombo vya habari juu ya masuala yanayohusu ofisi;

Kuratibu maandalizi ya nyaraka za kisekta;

Kuratibu maandalizi na uzalishaji wa makala za ofisi katika magazeti na majarida; na

Kuhuisha taarifa za kisekta kwenye tovuti




*Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu (kulia) akimkabidhi Mkuu wa Gereza la Mahabusu Segerea Mrakibu Mwandamizi wa Magereza Hamis Lissu, moja kati ya magodoro na vitu vingine ikiwemo mashuka, sabuni, mafuta na taulo za kike zilizotolewa na Shirika la Utangazaji nchini (TBC) kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa lengo la kuwasaidia Watoto waliopo katika Vizuizi vya Kisheria ambao wanatunzwa katika Gereza la Segerea Jijini Dar es Salaam.*




*Picha ya pamoja ikijumuisha Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Bw. Sylvester Mwakitalu (aliyekaa katikati), Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Joseph Pande (aliyekaa kushoto), Mkurugenzi wa Idara ya Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi Bw. Tumaini Kweka (aliyekaa kulia) wakiwa na Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa walioshiriki kwenye Kikao kazi cha Menejimenti na Wakuu wa Mashtaka wa Mikoa kilichofanyika Jijini Dodoma.*

# OFISI ZA MASHTAKA ZA MIKOA

## MAJUKUMU

Kutoa huduma za kimashtaka mkoani ikiwa ni pamoja na kufungua, kuendesha au kuondoa mashtaka yaliyofunguliwa kwa minajili ya kutenda haki, maslahi ya umma na kuzuia ukiukaji wa taratibu za kisheria;

Kuratibu upelelezi na kutoa muongozo kwa taasisi zinazotekeleza sheria kwenye makosa ya udanganyifu, rushwa na mengine yanayohusiana nayo;

Kuandaa hati za mashtaka, maombi na nyaraka nyingine zinazoendeana na haya;

Kusimamia kesi za rushwa zinazoshughulikiwa na mamlaka nyingine zinazopambana na rushwa na udanganyifu;

Kufanya mapitio ya majalada toka vyombo chunguzi;

Kutoa ushauri kwa taasisi zinazotekeleza sheria kwenye makosa dhidi ya binadamu na mamlaka za umma;

Kushughulikia kesi za vifo vya mashaka;

Kushughulikia kesi za rufaa na maombi katika mahakama za juu;

Kushughulikia mashahidi kabla, wakati wa kusikiliza kesi na baada ya kutoa ushahidi mahakamani;

Kusimamia kesi zinazohusu makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu na madawa ya kulevya, ndani ya mamlaka yao;

Kutoa mwongozo, kufungua na kuendesha kesi zinazohusiana na utaifishaji na urejeshaji wa zana zinazotumika katika uhalifu na mazalia yake;

Kuratibu kwa kushirikiana na wadau wa haki jinai, kurejesha na kutaifisha mali haramu ndani ya mamlaka yao;

Kuunganisha ofisi ya mashtaka na taasisi nyingine zinazoendesha mashtaka mkoani kwa lengo la kuhakikisha ufanisi katika upepelezi unaoratibiwa na Mwendesha Mashtaka;

Kufanya ukaguzi sero za polisi na magereza;

Kuwezesha kamati za usimamizi wa uendeshaji kesi katika ngazi ya mkoa na wilaya na majukwaa mengine;

Kuandaa na kuchambua data za kesi za jinai;

Kutunza kanzi data na mfumo wa taarifa wa mashtaka;

Kuelimisha umma kuhusu utenganiishaji wa upelelezi na uendeshaji wa mashtaka;

Kutekeleza na kusimamia kanuni za nidhamu za Waendesha Mashtaka;

Kuratibu uchukuaji wa waendeshaji wa mashtaka toka taasisi chunguzi mkoani;

Kuanzisha na kutunza taarifa za Waendesha Mashtaka wote mkoani;

Kuratibu na kuongoza taasisi zinazotekeleza sheria za makosa ya mazingira, kimtandao na makosa mengine yanayoendana na hayo;

Kusimamia kesi za kimazingira na kimtandao zinazoendeshwa na mamlaka nyingine;

Kushughulikia maswala ya kiutawala, kifedha na kiutumishi katika mamlaka yao;

Kufanya utafiti katika uendeshaji wa kesi za jinai ili kuhakikisha sheria, kanuni, amri, taratibu na miongozo yote iliyokwishatolewa inafuatwa; na

Kukagua na kufatilia uendeshaji wa kesi katika ofisi za mashtaka za wilaya ili kuhakikisha unafanyika kwa ufanisi.

# WAKUU WA MASHTAKA MKOA



**NDG. ABEL MWANDALAMA**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Mara



**NDG. MERCY NGOWI**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Singida



**NDG. ABDALLAH CHAVULA**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Arusha



**NDG. CASTUS NDAMUGOBA**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Geita



**NDG. WAZIRI MAGUMBO**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Kagera



**NDG. KHALILI NUDA**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Kilimanjaro



**NDG. ESTER MARTIN**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Lindi



**NDG. CHEMA MASWI**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Manyara



**NDG. VENANCE MAYENGA**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Katavi



**NDG. SARAJI IBORU**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Dar es Salaam



**NDG. NEEMA C. HAULE**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Morogoro



**NDG.JOSEPH J. MAUGGO**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Mtwara



**NDG. JANETHREZA A. KITALY**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Kinondoni



**NDG. APIMARK MABROUK**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Ilala



**NDG. BIBIANA KILEO**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Mwanza



**NDG. MKUNDE MSHANGA**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Pwani



**NDG. PASCHAL MARUNGU**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Rukwa



**NDG. KAULI G. MAKASI**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Ruvuma



**NDG. SHABAN MWEGOLE**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Simiyu



**NDG. NJOLOYOTA MWASHUBILA**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Songwe



**NDG. UPENDO J. MALULU**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Tabora



**NDG. ACHILES MULISA**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Njombe



**NDG. AJUAYE B. ZEGELI**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Shinyanga



**NDG. BASILIUS NAMKAMBE**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Iringa



**NDG. CATHERINE GWALTU**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Dodoma



**NDG. AHMED SEIF**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Mbeya



**NDG. ERASTO ANOSISYE**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Kigoma



**NDG. ANUNCIATHA LEOPOLD**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Temeke



**NDG. SHOSE NAIMAN**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Tarime



**NDG. JUMA MAIGE**

Mkuu wa Mashtaka Mkoa wa Tanga



*Picha ya pamoja ikijumuisha Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu (aliyekaa katikati), Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Joseph Pande (aliyekaa wapili kushoto), Mkurugenzi Msaidizi wa Utawala Bw. Leonard Mehta (aliyekaa wapili kulia), Mkurugenzi Idara ya Usimamizi wa Kesi na Uratibu wa Upelelezi Bi. Neema Mwanda (aliyekaa wakwanza kushoto), wakiwa na washiriki wa kikao kazi ambao ni Wakuu wa Mashtaka Mikoa kilichofanyika Jijini Dodoma*

# OFISI ZA MASHTAKA ZA WILAYA

## MAJUKUMU

Kutoa huduma za kimashtaka wilayani ikiwa ni pamoja na kufungua, kuendesha au kuondoa mashtaka yaliyofunguliwa kwa minajili ya kutenda haki, maslahi ya umma na kuzuia ukiukaji wa taratibu za kisheria;

Kuratibu upelelezi na kutoa muongozo kwa taasisi zinazotekeleza sheria kwenye makosa ya udanganyifu, rushwa na mengine yanayohusiana nayo;

Kuandaa hati za mashtaka, maombi na nyaraka nyingine zinazoendeana na haya;

Kusimamia kesi za rushwa zinazoshughulikiwa na mamlaka nyingine zinazopambana na rushwa na udanganyifu;

Kufanya mapitio ya majalada toka vyombo chunguzi;

Kutoa ushauri kwa taasisi zinazotekeleza sheria kwenye makosa dhidi ya binadamu na mamlaka za umma;

Kushughulikia kesi za vifo vya mashaka;

Kushughulikia kesi za rufaa na maombi katika mahakama za juu;

Kushughulikia mashahidi kabla, wakati wa kusikiliza kesi na baada ya kutoa ushahidi mahakamani;

Kusimamia kesi zinazohusu makosa ya usafirishaji haramu wa binadamu na madawa ya kulevya, ndani ya mamlaka yao;

Kutoa mwongozo, kufungua na kuendesha kesi zinazohusiana na utaifishaji na urejeshaji wa zana zinazotumika katika uhalifu na mazalia yake;

Kuratibu kwa kushirikiana na wadau wa haki jinai, kurejesha na kutaifisha mali haramu ndani ya mamlaka yao;

Kuunganisha ofisi ya mashtaka na taasisi nyingine zinazoendesha mashtaka wilayani kwa lengo la kuhakikisha ufanisi katika upelelezi unaoratibiwa na Mwendesha Mashtaka;

Kufanya ukaguzi sero za polisi na magereza;

Kuwezesha kamati za usimamizi wa uendeshaji kesi katika ngazi ya wilaya na majukwaa mengine;

Kuandaa na kuchambua data za kesi za jinai;

Kutunza kanzi data na mfumo wa taarifa wa mashtaka;

Kuelimisha umma kuhusu uchukuaji na uendeshaji wa mashtaka;

Kutekeleza na kusimamia kanuni za nidhamu za Waendesha Mashtaka

Kuratibu uchukuaji wa waendeshaji wa mashtaka toka taasisi chunguzi wilayani;

Kuanzisha na kutunza taarifa za Waendesha Mashtaka wote wilayani;

Kuratibu na kuongoza taasisi zinazotekeleza sheria za makosa ya mazingira, kimtandao na makosa mengine yanayoendana na hayo;

Kusimamia kesi za kimazingira na kimtandao zinazoendeshwa na mamlaka nyingine;

Kushughulikia maswala ya kiutawala, kifedha na kiutumishi katika mamlaka yao; na

Kufanya utafiti katika masuala ya jinai na uendeshaji wa kesi zake ili kuhakikisha sheria, kanuni, amri, taratibu na miongozo yote iliyokwishatolewa inafuatwa.

# MATUKIO KATIKA PICHA




*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan (aliyeketi katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Viongozi mbalimbali walioshiriki kwenye Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali uliofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma, wakwanza kulia aliyesimama ni Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu.*



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akisalimiana na Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu alipowasili kushiriki kwenye Mkutano Mkuu wa Chama cha Mawakili wa Serikali uliofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Jakaya Kikwete Jijini Dodoma.*






*Wanawake watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakisherekea Siku ya Wanawake Duniani ambayo kitaifa ilifanyika Jijini Dodoma.*




*Picha ya pamoja ikijumuisha Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu (katikati), akiwa na baadhi ya watumishi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Makao Makuu Jijini Dodoma na Mkoa wa Tabora, Jeshi la Magereza na Polisi walipotembelea Gereza Kuu Uyui Mkoani Tabora alipokuwa kwenye ziara ya kutembelea Magereza nchini.*




*Picha ya pamoja ikijumuisha Mkurugenzi wa Divisheni ya Makosa ya Udanganyifu, Utakatishaji Fedha na Rushwa kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw.Oswald Tibabyekomya (wapili kushoto), Mkuu wa gereza la Wilaya ya Manyoni Mrakibu Mwandamizi wa Magereza Bakari Sudi (wa kwanza kushoto) wakiwa na baadhi ya viongozi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pamoja na Jeshi la Magereza na Polisi walipotembelea gereza la Wilaya ya Manyoni Mkoani Singida walipokuwa kwenye ziara ya kutembelea Magereza nchini.*



*Picha ya pamoja ikijumuisha Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dodoma Mhe. Dkt. Adam Mambi (katikati), Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dodoma Mhe. George Masaju (watatu kushoto), Jaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Dodoma Mhe. Dkt. Fatma Halfan (watatu kulia), Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitatu (wapili kushoto) wakiwa na Waendesha Mashtaka pamoja na Wapelelezi walioshiriki kwenye mafunzo yaliyofanyika Jijini Dodoma*



*Washiriki wa Mafunzo ya Waendesha Mashtaka na Wapelelezi wakifuatilia kwa umakini mada mbalimbali zilizowasilishwa kwenye mafunzo hayo yaliyofanyika Jijini Dodoma*



**Shedrack Kimaro**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utaifishaji na Urejeshaji Mali

# Utaifishaji na Urejeshaji wa Mali Zitokanazo na Uhalifu

Makala

## UTANGULIZI

Kuongezeka kwa uhalifu wa kupangwa (organised crime) unaofanywa kwa lengo la kujipatia mali kama vile biashara haramu ya dawa za kulevya katika miaka ya 1980 kulisababisha athari kubwa za kiuchumi na kijamii. Ili kukabiliana na uhalifu huo, hatua mbali mbali zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na adhabu kali za vifungo kuwekwa kwa wahalifu wa makosa hayo. Licha ya hatua hizo kuchukuliwa, uhalifu huo ulizidi kukithiri na kuwa tishio kubwa la usalama kwa nchi mbali mbali duniani ikiwemo Tanzania. Ongezeko la vitendo hivi kulidhihirisha kuwa jitihada za kupambana na uhalifu kwa kuwafunga wahalifu gerezani, huku wakiendelea kufaidika na matunda ya uhalifu wao mara baada ya kumaliza kutumikia adhabu zao, kusingeweza kupunguza uhalifu unaotendeka kwa lengo la kupata mali. Kutokana na hali hii, nchi nyingi na jumuiya za kimataifa ziliazimia na kuweka mkakati wa kupambana na uhalifu wa namna hii kwa lengo la kumnyima mhalifu fursa ya kufaidika na matunda ya uhalifu kwa kurejesha mali zinazopatikana kutokana na vitendo vya uhalifu.

Kwa mara ya kwanza Tanzania ilichukua hatua katika mkakati wa urejeshwaji wa mali zinazotokana na uhalifu kama njia ya kuzuia uhalifu wa mali mwaka 1991. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na Bunge kutunga Sheria ya Mazalia ya Uhalifu, Sura 256 (The Proceeds of Crime

Act, Cap. 256) na hivyo kuweka mfumo wa kisheria wa kusimamia urejeshwaji wa mali zinazohusiana na uhalifu. Madhumuni ya Sheria yalilenga kuzuia vitendo vya kujipatia mali kwa njia ya uhalifu kwa kuwanyima wahalifu fursa ya kufaidika na mali za aina hiyo na pia kuhakikisha kuwa waathirika wa vitendo vya uhalifu (Victims of Crime) wanarejeshewa mali zao. Sheria hii pia iliweka masharti ya kuvipatia vyombo vya uchunguzi mamlaka ya kuchunguza mali zinazohusiana na makosa ya jinai na kuweka utaratibu wa kisheria wa kuzuia na kurejesha mali zinazohusiana na makosa hayo. Kwa mujibu wa Sheria hii, mali zinazoweza kurejeshwa ni zile ambazo zinatokana au zimetumika kutenda makosa ya uhalifu (tainted properties).

Misingi ya kutungwa kwa sheria hii ipo katika Katiba ya nchi, sera na mikataba ya kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia pamoja na vigezo vya kimataifa vya kupambana na utakatishaji wa fedha na ufadhili wa ugaidi. Ibara ya 27 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaweka wajibu wa kulinda mali za umma na mtu binafsi dhidi ya vitendo vya uhalifu. Aidha, Mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ikiwemo Makubaliano ya Harare ya mwaka 1986, Mkataba wa wa Kimataifa dhidi ya Usafirishaji wa Dawa ya Kulevya wa mwaka 1988; Mkataba dhidi ya Makosa yanayovuka Mipaka wa Mwaka 2000; Mkataba wa Kimataifa wa Kupambana na Rushwa wa Mwaka 2003 na Vigezo vya Kimataifa vya Kudhibiti Utakasishaji Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi (FATF Recommendations, 2022) imeweka masharti kwa nchi wanachama kutunga sheria ya kurejesha mali zinazohusiana na uhalifu kama mkakati wa kudhibiti makosa ya yanayotendeka kwa ajili ya kupata mali.

## UTEKELEZAJI WA SHERIA

Sheria ya Kutaifisha Mazalia ya Uhalifu, Sura ya 256, ilitangazwa katika Gazeti la Serikali mwaka 1994. Pamoja na kutangazwa kwa sheria hiyo, haikuanza kutumika hadi mwaka 2011 Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilipoanza rasmi kuitumia sheria hiyo. Mwaka 2012, muda mfupi baada ya kuanza kutumika, Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho makubwa kutokana na upungufu uliojitokeza mara baada ya kuanza kutumika na pia upungufu uliobainishwa katika taarifa ya Tathmini ya Tanzania ya Mifumo ya Kitaasisi na Kisheria kuhusu udhibiti wa utakatishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi iliyofanywa na Umoja wa Kudhibiti Utakatishaji wa Fedha Haramu (Eastern and Southern African Anti Money Laundering Group (ESAAMLG) kwa nchi za Mashariki na Kusini mwa Afrika ya mwaka 2009.

Baada ya marekebisho hayo, Serikali imechukua hatua mbalimbali katika kuitekeleza Sheria hiyo. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:

i. Kuanzishwa kwa Sehemu ya Utaifishaji na Urejeshwaji Mali Zinazohusiana na Uhalifu katika Muundo wa Iliyokuwa Kurugenzi ya Mashtaka katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali mwaka 2011;

ii. ufunguaji wa jumla ya maombi 53 ya uzuiaji na urejeshwaji wa mali mahakamani (Restraint and Forfeiture Applications) kati ya mwaka 2011 na 2022;

iii. Kufungua akaunti maalum kwa ajili ya kuweka fedha zinazotokana na mali zilizorejeshwa, inayojulikana kama *Asset Forfeiture and Recovery Account* katika Benki Kuu ya Tanzania.

Utekelezaji wa hatua hizo uliwezesha kurejeshwa kwa shilingi za ki-Tanzania 16,040,133,359.22 na Dola za Marekani 7,741,633.92 taslimu na mali za aina mbalimbali zikiwemo nyumba, viwanja, na vyombo vya usafiri zinazokadiriwa kuwa na thamani ya zaidi ya shilingi za kitanzania bilioni 7. Aidha, madini ya dhahabu kilogramu 453, almasi carats 71,654.45 na madini mengine ya vito kama Tanzanite yenye na thamani ya 101,483,106,126.05 yalitaifishwa kuwa mali ya Serikali.

Pamoja na mafanikio hayo zipo changamoto ambazo zinaathiri utekelezaji wa sheria hii kwa ujumla wake. Changamoto hizo ni pamoja na:

i. Kukosekana kwa utaratibu wa kisheria wa kusimamia (asset management), kuondosha na matumizi ya mali zilizorejeshwa (disposal); na

ii. Kukosekana kwa mwongozo wa matumizi ya fedha katika Akaunti inayohifadhi fedha zilizotokana na mali za uhalifu;

## UZOEFU TOKA NCHI NYINGINE

Uzoefu kutoka nchi za Botswana, Kenya na New Zealand unaonyesha mafanikio katika kushughulikia baadhi ya changamoto hizi. Nchi hizi zimeweka mifumo na taratibu za kisheria katika sheria husika ili kuimarisha mapambano katika makosa yanayohusu mali zilizopatikana kwa njia za uhalifu. Kwa mfano Sheria ya Urejeshwaji wa Mali Zilizopatikana kwa njia ya Uhalifu ya Mwaka 2013 ya Kenya:

i. inaanzisha taasisi kwa ajili ya kutekeleza sheria ya urejeshwaji mali ikiwemo kufungua maombi ya kuzuia au kurejesha mali mahakamani;

ii. inaanzisha mfuko (Asset Recovery Fund) kwa ajili ya kuweka fedha zinzotokana na mali zilizorejeshwa;

iii. inaruhusu kufunguliwa akaunti kwa ajili ya kutunza fedha zinazokamatwa wakati wa utekelezaji wa sheria; na

iv. inaweka utaratibu wa madai wa kurejesha mali zinazohusiana na uhalifu katika mazingira ambayo mtuhumiwa hawezi kushughulikwa kwa njia za kijinai (Civil Forfeiture).

Vile vile nchini Botswana, Sheria ya Urejeshwaji wa Mali Zilizopatikana kwa njia ya Uhalifu ya Mwaka 2007:

i. inaanzisha Taasisi iitwayo *Office of Receiver* kwa ajili ya kusimamia

na kuhifadhi mali zilizozuiliwa na zilizotaifishwa;

ii. inaanzisha mfuko (*Confiscated Asset Trust Fund)* kwa lengo la kuweka fedha zinazotokana na mali zilizorejeshwa; na

iii. inaweka utaratibu wa kurejesha mali zinazohusiana na uhalifu katika mazingira ambayo mtuhumiwa hawezi kushughulikiwa kwa njia za jinai (Civil Forfeiture).

Sheria ya Urejeshwaji wa Mali zilizopatikana kwa njia ya Uhalifu ya mwaka 2009 ya New Zealand kwa upande wake:

i. inaweka masharti ya kutumia taasisi ya Serikali-*Official Assignee* kusimamia na kuhifadhi mali zilizozuiliwa na kurejeshwa;

ii. inaweka utaratibu wa kuuzwa mali wakati wa kusubiri amri ya urejeshwaji mali kwa ajili ya kuhakikisha mali hazipotezi thamani; na

iii. inaweka utaratibu wa kurejesha mali zinazohusiana na uhalifu katika mazingira ambayo mtuhumiwa hawezi kufikishwa mahakamani (Civil Forfeiture).

Aidha, makubaliano na mikataba mbalimbali ya kimataifa inayohusu urejeshwaji wa mali zinazohusiana na uhalifu inatoa mwongozo wa kushughulikia changamoto hizi kwa kuweka mifumo na taratibu za kushughulikia masuala haya katika sheria za nchi.

## HALI ILIVYO KWA SASA

Licha ya kutungwa mwaka 1991, Sheria ya Kutaifisha Mazalia ya uhalifu, Sura ya 256, ilianza kutekelezwa mwaka 2011. Miongoni mwa hatua za utekelezaji wa Sheria ni kuanzishwa Sehemu ya Utaifishaji Mali na Urejeshwaji wa Mali zinazohusiana na Uhalifu katika iliyokuwa Kurugenzi ya Mashtaka chini ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hatua hii ilienda sambamba na kupanga mawakili wa kufanya kazi katika Sehemu hiyo ambao walipatiwa mafunzo maalum ya urejeshwaji wa mali zinazotokana na uhalifu ndani na nje ya nchi.

Mwaka 2018, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ilianzishwa ikiwa na Divisheni 5 ikiwepo Divisheni ya Utaifishaji Mali, Makosa yanayovuka Mpaka na Uhalifu Makhususi. Divisheni hii ina sehemu tatu ikiwemo Sehemu ya Utaifishaji na Urejeshaji Mali zinzohusiana na Uhalifu.

Majukumu ya Sehemu hii ni pamoja na kufungua na kuendesha maombi ya urejeshwaji wa mali mahakamani, kuratibu upelelezi wa mali zinazohusiana na uhalifu, kufuatilia na kushauri juu ya utekelezaji wa amri za mahakama za kuzuia au kurejeshwa mali, kutoa mapendekezo ya maboresho ya sheria na kufungua na kuendesha maombi ya kusajili amri za kuzuia au kurejesha mali zilizotolewa nje ya nchi kwa ajili ya kutekelezwa hapa nchini.

Kufikia mwezi Januari, 2022, jumla la madini yenye thamani ya Shillingi 101,483,106,126.05,

magari 175, nyumba 44 , pikipiki 73 na fedha taslimu shilingi 16,040,133,359.22 na dola za Kimarekani 7,741,633.92 zilitaifishwa na kuwa mali ya Serikali. Baadhi ya mali hizo zilizotaifishwa zilikabidhiwa kwa Katibu Mkuu Hazina. Baada ya makabidhiano, magari 147 yaligawiwa kwa jumla ya taasisi 24 za Serikali. Taasisi hizo ni, Ofisi za Maafisa Tawala za wilaya 27, Jeshi la Kujenga Taifa, Ofisi ya Rais Tume ya Ajira, Jeshi la Wananchi wa Tanzania, TANESCO, Jeshi la Polisi, VETA, PSU, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Ikulu, Usalama wa Taifa, Mamlaka ya Kuzuia na Kupambana na Dawa za Kulevya, Temesa, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali, Jeshi la Magereza, Mahakama, Idara ya Uhamiaji, Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Nyamagana, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege na TSN.

Fedha taslimu zinazotaifishwa huwekwa kwenye akaunti maalum namba 9931209531 ya Dola za Marekani na 9921161271 ya shilingi za Kitanzania zilizopo Benki Kuu ya Tanzania kwa jina la *Asset Forfeiture and Recovery Account.* Akaunti hii ilifunguliwa kama hatua ya dharura kutokana na kutokuwepo utaratibu uliowekwa kisheria kushughulikia fedha zinazopatikana katika utekelezaji wa sheria hii. Hata hivyo, akaunti hii mpaka sasa haijatambuliwa kisheria.

Pamoja na hatua mbalimbali zilizochukuliwa na mafanikio yaliyopatikana zimekuwepo changamoto zinazoathiri utekelezaji wa sheria na misingi yake. Changamoto hizo ni pamoja na:

i. **Kutokuwepo kwa utaratibu wa kusimamia, na kutumia mali zilizorejeshwa** - Sheria haijaweka utaratibu madhubuti wa kusimamia mali (asset management), na kutumia (asset allocation) mali zilizorejeshwa. Ingawa Sheria inampatia Katibu Mkuu Hazina mamlaka ya kumiliki mali zilizotaifishwa kuwa mali ya Serikali, haikuweka utaratibu wa matumizi ya mali hizo tofauti na hali ilivyo kwenye mataifa mengine.

ii. **Kukosekana mwongozo wa kuendesha akaunti ya kuweka fedha zilizorejeshwa -** Sheria haijaanzisha mfuko wa kuweka fedha zinazorejeshwa au kupatikana kutokana na mauzo ya mali zilizorejeshwa. Kutokana na upungufu uliojitokeza wakati wa utekelezaji wa sheria, ilifunguliwa akaunti Benki Kuu ya Tanzania kwa ajili ya kuweka fedha zinazopatikana kutokana na mali zilizorejeshwa. Hata hivyo, hakuna mwongozo wa kisheria wa namna ya kuendesha na kutumia fedha zilizopo katika akaunti hiyo utakaohakikisha uwazi na uwajibikaji katika matumizi ya fedha hizo. Kutokana na upungufu huo fedha zilizopo katika akaunti hiyo hazitumiki. Katika ukurasa wa 41 wa Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na

Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka wa fedha ulioshia tarehe 30 Juni 2020, CAG alibainisha kuwa:-

*"kutotumiwa kwa Bakaa ya fedha katika akaunti kunasababishwa na kutokuwapo kwa sheria na kanuni za kudhibiti matumizi ya fedha itokanayo na mali zilizotaifishwa na kurejeshwa Serikalini."*

Na hivyo CAG alitoa ushauri ufuatao:-

*"Ninapendekeza kuwa, Serikali kutunga sheria ya ugawaji na matumizi ya Fedha katika akaunti ya unyakuzi na uokoaji".*

iii. **Kutokuwepo utaratibu wa kumfidia mhanga wa uhalifu.** – Sheria inaelekeza mali zote zinazotaifishwa kuwa mali ya Serikali. Hata hivyo, Sheria haijatoa mwanya au mwongozo pale ambapo mali husika inastahili kutaifishwa na kuwa mali ya mhanga wa uhalifu (Victim of Crime).

Kwa kuzingatia changamoto tajwa, inapendekezwa kuwa njia pekee ya kuzitatua changamoto zilizobainishwa ni kufanyika kwa marekebisho ya sheria ya Urejeshwaji wa Mali Zinazotokana na Uhalifu, Sura ya 256 ili kuziondoa au kuzipunguza changamoto hizo kwa lengo la kuimarisha mfumo wa kisheria wa urejeshwaji wa mali zinazohusiana na uhalifu kutoka kwa wahalifu.



*Baadhi ya Waendesha Mashtaka na Wapelelezi kutoka Mikoa na Wilaya mbalimbali nchini wakimsikiliza Bw. Shedrack Kimaro (hayupo pichani) ambaye ni Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utaifishaji na Urejeshaji Mali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakati akitoa mada juu ya Utaifishaji Mali zitokanazo na Uhalifu, Sheria na Utaratibu yaliyofanyika jijini Mwanza.*



**Ignas Joseph Mwinuka**
Wakili wa Serikali Mwandamizi

# Ulinzi wa Mashahidi Katika Mfumo wa Haki Jinai

Makala

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inalo jukumu la kisheriala kuwalinda mashahidi na jukumu hili linasimimiwa na Divisheni ya Usimamizi wa Kesi na Uratibu wa Upelelezi (Case Management and Coordination of Criminal Case Division) Kwanini kuna hitaji la kuwalinda mashahidi? Kama mwanafalsafa wa sheria Jeremy Bentham alivyosema: "mashahidi ni macho na masikio ya haki" hivyo ni sehemu muhimu katika mchakato mzima wa kesi. Kama shahidi hatakuwa macho na masikio ya haki kesi itaharibika ama kupooza na hii haiwezi tena kuwa kesi iliyosikilizwa kwa misingi ya haki(fair trial) kama ilivyoamriwa katika mahakama ya upeo ya India katika shauri la Zahira Habibulla H. Shiekh and Another v. State of Gujarat mahakama ilisema kesi itakuwa haijasikilizwa katika misingi ya haki (fair trial) iwapo mashahidi watapata vitisho na kulazimika kutoa ushahidi wa uongo". Mashahidi hushindwa kutoa ushahidi wa kweli mahakamani kutokana na sababu zilizo nje ya uwezo waokama ujinga, uzembe na njama za wahalifu.

Changamoto zinazowakabili mashahidi wa upande wa mashtaka Jaji AK wa Mahakama Upeo ya India (Supreme Court) anataja changamoto saba zinazowakabili mashahidi, ambazo huwafanya mashahidi wasitoe ushahidi wa kweli na kugeuka na kuwa mashahidi vigeugeu (Hostile witness) sababu hizo ni;-

- Vitisho
- Ushawishi kwa njia mbali mbali.
- Hongo toka kwa watuhumiwa.
- Shahidi mmoja kutumika kutoa

ushahidikatika kesi nyingi.

- Ucheleweshaji wa usikilizwaji wa kesi.
- Kadhia zilizowakumba mashahidi wakatiwa upelelezi wa kesi.
- Udhaifu wa mifumo ya kisheria katika kuwalinda mashahidi.

**Hatua za ulinzi wa mashahidi.**

Hatua za ulinzi wa mashahidi zinaweza kutazamwa kwa misingi ya kesi kwa kesi hasa kwa kungalia mazingira hatarishi ya shauri husika.

Hatua za usalama za mashahidi ziko katika makundi matatu;-

- Hatua za ulinzi kutoka vyombo chunguzi,
- Hatua za kimahakama, na
- Uwepo wa programu mahususi wa ulinzi wa mashahidi.

**Hatua za Ulinzi kutoka vyombo Chunguzi**

Mazoea mazuri ya uchunguzi/upelelezi ni pamoja na kuweka upelelezi kuwa siri na kuhakikisha kwamba taarifa zote kuhusu historia ya mtuhumiwa wa uhalifu, hasa kuhusiana na vurugu, mahusiano na makundi ya wahalifu, na vitendo vyovyote vya vitisho vinavyotolewa kwa mashahidi

vinafahamishwa kwa Waendesha Mashtaka na Majaji hasa wakati wa dhamana.

Mambo mengine yanayoweza kufanywa katika hatua hii ni pamoja na Msaada wa kisaikolojia, Kuwalinda mashahidi wanapoingia mahakamani kutoa ushahidi, Kuhakikisha hawaandaliwi mbele ya umma na jamaa ya watuhumiwa, Mashahidi kujulikana siku ya kesi, kubadilisha makazi,kubadilisha mawasiliano ya simu,mashahidi kutumia vifaa vya usalama na kutumia majengo ya faragha katika kuwahoji na kuwaandaa mashahidi.

Mfumo wa kisheria katika nchi yetu katika hatua hii, unaangaziwa na kifungu cha 53(1) cha Sheria ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa Sheria inaelekeza inapojidhihirisha kuwa kuna hatari ya kesi kuharibiwa kutokana na vitisho kwa mashahidi na mali zao, Inspekta Jenerali wa Polisi kwa uamuzi wake mwenyewe ama baada ya kushauriana na Mkurugenzi wa Mashtaka , Kuchukua hatua za kuwalinda mashahidi na familia zao.

**Hatua za kimahakama**

Hizi ni hatua zinazochukuliwa na mahakama kum linda shahidi wakati akitoa ushahidi wake mahakamani ili kuhakikisha kuwa shahidi anatoa ushahidiwake bila vitisho au hofu ya maisha yake, kwa uchache mambo yanayoweza kufanywa katika hatua hii ni pamoja na kuficha utambulisho wa shahidi, shahidi kutoa ushahidi kwa kutumia Video ( video conferencing), Kutumia vifaa vya kubadilisha sauti na sura (voice and face distortion techniques).

Katika mfumo wa Sheria wa Nchi yetu, hatua hii inaakisiwa na Kifungu cha 188 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai ambacho kinaruhusu Mkurugenzi wa Mashtaka kufanya maombi pasipo mtuhumiwa kuwapo (exparte) ili kupata amri ya mahakama ya

kuwalinda mashahidi. Aidha katika kanuni za Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa katika aya ya 21 inatoahaki kwa pande zote ya Mashtaka na utetezi kuwasilisha maombi ya kuwalinda mashahidi.

**Hatua ya Uanzishwaji wa Mpango Mahsusi (Scheme)**

Huu ni mpango mahususi (scheme) wa kuratibu ulinzi wa mashahidi ambao maisha yao yanatishiwa na kikundi cha uhalifu kwa sababu ya ushirikiano wao na mamlaka ya kutekeleza sheria.

**Vigezo vya kuzingatia katika kuwalinda mashahidi**

Vigezo vya kuzingatiwa katika kufanya maamuzi na kuchukua hatua ya kuwalinda mashahidi ni kama ifuatavyo:

1. Aina ya mazingira ya uhalifu (uhalifu uliopangwa, uhalifu wa kijinsia, uhalifu wa kifamilia n.k)
2. Mazingira yanayomzunguka mhanga/ shahidi (mtoto, mwathirika wa unyanyasaji wa kijinsia, mshtakiwa mwenza n.k)
3. Uhusiano shahidi na mtuhumiwa (jamaa, mfanyakazi wa mshtakiwa katika genge la uhalifu nk)
4. Kiwango cha hofu na vitisho vilivyoelezewa kwa shahidi,
5. Uzito na umuhimu wake kwa ushahidi wake



*Picha ya pamoja inayojumuisha Wajumbe walioshiriki kwenye Mkutano wa Sekretarieti ya Jukwaa la Haki Jinai Taifa yaliyofanyika Jijini Dodoma.*



# Ijue Sheria na Miongozo ya Maamuzi ya Kushtaki

## Makala

**Rebecca Kwandu**

Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

Uamuzi wa kushtaki ni hatua muhimu katika mchakato wa haki ya jinai na unaongoza na kanuni za kisheria na za kimaadili kuamini kwamba ushahidi uliopo unatosha kuthibitisha hatia, licha ya uwepo wa utetezi wowote unaofaa, uonyeshe kwamba mshtakiwa ana hatia ya shtaka.

Aidha, ni vema kufahamu kwamba suala ya maamuzi ya kushtaki au kutoshitaki ndio moyo wakazi ya mashtaka.

Utaratibu uliopo ni kwamba, baada ya kupitia ush ahidi uliopo kwenye jalada la Polisi, Mwendesha Mashtaka anatakiwa kuandaa maoni ya kishe ria, yenye hoja za msingi za kisheria, ushahidi muhimu, mapungufu na hoja yeyote muhimu, na kupendekeza aina ya shtaka kulingana na ushahidi uliopo.

Maamuzi yote katika hatua hii ya kuamua kushtaki, huratibiwa katika kumbukumbu za kesi kwa taratibu za ndani za kiofisi na watu wasiohusika hawana nafasi kuyaona.

Kama mojawapo ya majukumu ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), katika kutekeleza mamlaka na utekelezaji wa majukumu yake, atazingatia yafua tayo:- (a) umuhimu wa kutenda haki (b) kutoingilia mchakato wa utoaji haki (c) maslahi ya umma na (d) kusimamia mienendo ya mashtaka. Aidha, wakati wa kutoa maamuzi ya kushtaki, Waendesha Mashtaka hawapaswi kuanzisha au kuendeleza mashtaka ambayo kwa maoni yao, upo uwezekano mkubwa mahakama ikaamua kwamba kufanya hivyo ni kuingilia mchakato wa utoaji haki nchini. Mnamo mwaka 2017, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) alitangaza utaratibu wa kiwango cha utendaji katika mfumo wa "Rapid Reference Guide (RRG)" ukitoa mwongozo wa utendaji kwa Waendesha Mashtaka na wapelelezi wa uhalifu wa wanyamapori na misitu. Kwa mfano,Mahakama Kuu ya Kenya, katika kesi

ya Cyrus Shakhalanga Khwa Jirongo dhidi ya Soy Developers Ltd na wengine 9 [2021] eKLR ilielekeza kwamba; "...katika kuanzisha mashtaka, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (ODPP), bila/kwa njia yoyote kuondoa mamlaka ya kikatiba ya kushtaki uhalifu, inapaswa kuchukua hatua kila wakati, kwa uadilifu na si kuchukua hatua katika kuende leza malalamiko ya jinai yasiyo ya haki na yenye nia mbaya.

Kwa kufanya hivyo, ofisi hii lazima siku zote iongozwe na kanuni kwamba usikilizwaji wa kesi kwa haki (fair trial), hauwezi kuwekewa kikomo na hili linapaswa kuzingatiwa wakati wa kuamua kushtaki au kutoshtaki.

Waendesha Mashtaka pia wanaweza kushauri au kuamua kesi nje ya mahakama kama njia mojawapo ya kumaliza kesi bila kufikishwa mahakamani kwa zile kesi ambazo sheria inaruhusu kufanya hivyo.

Waendesha Mashtaka wanapaswa kufanya maamuzi yao kwa mujibu wa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai, maagizo ya Mkuu wa Mashtaka kwa Waendesha Mashtaka na Mawakiliwa Serikali (PGI) 2008, maagizo Na. 1 ya mwaka 2017 na miongozo au sera yoyote husika

Pia, Waendesha Mashtaka wanatakiwa kuratibu, kusimamia na kushauri polisi na wapelelezi wengine kuhusu njia zinazofaa za uchunguzi, mahitaji ya ushahidi, taratibu za kabla ya kufunguliwamashtaka, usimamizi wa ufichuzi na mkakati wa jumla wa uchunguzi Hii inajumuisha maamuzi ya kuboresha au kupunguza upeo kuhusu tukio la kihalifu na idadi ya watuhumiwa wanaochunguzwa.

Katika ibara ya 59B(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977 kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kwa mara, ikisomwa pamoja na vifungu vya 16 (1) na 24(1)(2) vya Sheria ya Huduma ya Kitaifa ya Mashtaka, Sura 430, vinampa Mkurugenzi wa Mashtaka mamlakaya jumla ya kuanzisha, kuendesha na kusimamia mashtaka yote ya jinai nchini pamoja na kufanya kitu chochote muhimu kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu yake na hii ni pamoja na kuratibu upelelezi wa makosa ya jinai.

Waendesha Mashtaka pia wanapaswa kutambua na inapowezekana, kutafuta kurekebisha kasoro za ushahidi, lakini, kwa kuzingatia uzito au mazin gira ya kesi, wanapaswa kuacha haraka kuendelea na kesi ambazo hazina ushahidi wa kutosha na ambazo haziwezi kuimarishwa na uchunguzi zaidi au kama maslahi ya umma yanaonyesha kesi hiyo haitakiwi kuendelea.

Waendesha Mashtaka ndio hupitia kila kesi wanayopokea kutoka Polisi na vyombo vingine vya kiupelelezi.

Hata wakati kesi ikiwa tayari imefunguliwa mahakamani, Waendesha Mashtaka wanapaswa kuendelea kufuatilia mashtaka yaliyopo kwa kulin ganisha na sheria zinazohusika.

Uhakiki katika kesi ni mchakato unaoendelea na Waendesha Mashtaka lazima wazingatie mabadi liko yoyote yanayotokea wakati kesi ikiendelea.

Ikiwa kesi itafutwa, uangalifu unapaswa kuchukuliwa kuchagua njia bora ya kufanya hivyo, kwa sababu wakati mwingine inaweza kusababisha madhara kwenye maslahi ya mwathirika, taasisi au Serikali.

Wakati wowote inapowezekana, Waendesha Mashtaka wanapaswa kushauriana na mpelelezi wanapofikiria kubadilisha au kusitisha mashtaka.

Hata hivyo, pamoja na kwamba Waendesha Mashtaka na Wapelelezi hufanya kazi kwa karibu, jukumu la mwisho la uamuzi iwapo kesi inapaswakuendelea au la ni la Mwendesha Mashtaka au Ofisi ya Taifa ya Mashtaka (NPS).

## KESI ZINAZOHITAJI RIDHAA NA KIBALICHA DPP

Kuhusiana na kesi zinazohitaji kibali naridhaa kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka, Mwendesha Mashtaka lazima azingatie Tangazo la Serikali Na496H la 2021 na maagizo, au miongozo mingine yoyote ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) inayo husiana na makosa yanayohitaji ridhaa na kibali chake binafsi, au kama kuna ugatuzi wa madaraka kwa maofisa wanaofanya kazi chini yake.

Endapo ridhaa na kibali chake binafsi kitahitajika, lazima vitu hivyo vipatikane toka kwake, na ikiwa wapo maofisa wa ngazi fulani waliogatuliwamadaraka wanaofanya kazi kwa niaba yake, basihilo pia lizingatiwe na sheria husika zifuatwe.

Ikiwa mashtaka yanajumuisha mseto wa makosa ya uhujumu uchumi na yasiyo ya uhujumu uchumi, Mwendesha Mashtaka atahakikisha sheria mahsusi zinawekwa kwenye hati ya ridhaa na cheti vinavyoruhusu shitaka husika kuendeshwa katikamahakama za chini.

Endapo makosa ni ya uhujumu uchumi tu, kifungu sahihi ni 12(3) na kama ni mchanganyiko kifun gu sahihi ni 12(4) vya Sheria ya Uhujumu Uchumi na makosa ya kupangwa [sura ya 200 marejeo ya2019].

Waendesha Mashtaka pia wanapaswa kuwa huru katika utendaji wao wa kazi na hiyo ni sura ya jamii ya kidemokrasia inayofuata utawala wa sheria katika mfumo wa haki jinai.

Waendesha Mashtaka wanapaswa kuwa huru kutoka kwa watu au mashirika ambayo sio sehemu ya mchakato wa kufanya maamuzi ya mashtaka.

Aidha, Waendesha Mashtaka lazima wawe huru kutekeleza majukumu yao ya kitaaluma bila kuingiliwa kisiasa, na hawapaswi kuathiriwa na shinikizo au ushawishi usiofaa kutoka kwa chanzo chochote.

Si kazi ya Ofisi ya NPS, Wakili wa Serikali au Mwendesha Mashtaka wa Umma kuamua kama mtu ana hatia ya kosa la jinai. Jukumu lao kuu kama Maofisa wa Mahakama ni kuwasilisha shitaka na ushahidi ili kuisaidia Mahakama kufanya uchambuzi na kufikia maamuzi ya haki na usawa.

Mahakama pekee ndiyo yenye uwezo kumtamka mtu kama ni mkosaji. Na pia uamuzi wa kushitaki au kupendekeza kumaliza kesi nje ya mahakamaau kufungwa kwa jalada ni hatua kubwa inayowa gusa watuhumiwa, waathirika wa kosa, mashahidi na jamii kwa ujumla hivyo ni lazima ufanywe kwa uangalifu mkubwa.

Ni wajibu wa Waendesha Mashtaka kuhakikisha mtuhumiwa aliyepo ni mtu sahihi kwa tuhuma husika kwa mujibu wa ushahidi na anatakiwa kushitakiwa kwa kosa sahihi na la haki. Watuhumiwa wote ambao

ushahidi unawagusa, lazima wafikishwe mbele ya vyombo vya kutoa haki wakati wowote itakapowezekana.

Maamuzi ya kesi yanayochukuliwa kwa haki, bilaupendeleo na kwa uadilifu husaidia kupata haki kwa waathirika, mashahidi, watuhumiwa, washitakiwa na jamii husika.

Waendesha Mashtaka lazima wahakikishe kwam ba katika utendaji wao, sheria sahihi inatumika ipasavyo, na kuleta ushahidi unaofaa mbele ya Mahakama.

Wakati wa kufanya maamuzi ya kushtaki, Waende sha Mashtaka lazima wawe waadilifu na wenye malengo ya kutafuta haki na hawapaswi kuruhusu maoni yoyote ya kibinafsi kuhusu asili ya kabila, Taifa, jinsia, ulemavu, umri, dini au imani na mam bo mengine yoyote yanayoweza kuathiri upatikanaji wa haki katika maamuzi yao.

Pamoja na hayo, hawapaswi kuhamasishwa na mazingatio ya kisiasa. Utendaji wa Waendesha Mashtaka lazima siku zote uendane na sheria na kwa maslahi ya haki na sio tu kwa madhumuni yakushinda kesi.

Katika kesi zote zinazopita mikononi mwao, Waendesha Mashitaka hawatakiwi kuwa na upendeleo wowote na wana wajibu wa kulinda haki za watuhumiwa na washtakiwa, huku wakitoa huduma bora zaidi kwa waathirika wa tukio.

Katika kuamua kushtaki au kutoshtaki, Mwendesha Mashtaka au Wakili wa Serikali ataongozwa na maslahi ya umma (pamoja na maslahi ya haki). Umuhimu wa kuepusha kuingilia mchakato wa utoaji haki na uwepo wa matumaini ya kushinda kesi, vyote kwa pamoja vyaweza kuelezwa kwa tathimini zifuatazo hapa chini, hasa kwa kuzingatia vigezo viwili ambavyo ni uwepo wa ushahidi thabiti na maslahi ya umma.

## KIPIMO CHA UWEPO WA USHAHIDI

Kabla ya kuamua kufungua mashtaka Mahakamani, Mawakili wa Serikali pamoja na Waendesha Mashtaka lazima wajiridhishe kwamba upo ushahidi wa kutosha kumtia hatiani mtuhumiwa.

Wanatakiwa pia kuzingatia utetezi unaoweza kuletwa na mshitakiwa na mazingira yanayoweza kupelekea kesi yao kushindwa.

Kesi ambayo haikidhi vigezo vya kipimo cha ushahidi haitakiwi kuendelea. Inatakiwa aidha irudish we kwa ajili ya upelelezi zaidi kama ni muhimu ku fanya hivyo, au ifutwe kama hakuna viashiria vya mafanikio ya kupata ushahidi wa ziada.

Wakati wa kuamua kama kuna ushahidi wa kutosha kushtaki, Waendesha Mashtaka wanapaswa kujiuliza mambo yafuatayo:-

1. Je? Ushahidi unaweza kupokelewa mahakama ni? Je, Kuna swali lolote juu ya kukubalika kwa ushahidi fulani.
2. Ushahidi huo una uhalisia wowote? Je, kuna sababu zozote za kutilia mashaka uhalisia waushahidi huo.
3. Je, ushahidi huo ni wa kuaminika. Je, kuna sababu zozote za kutilia shaka kuaminika kwa ushahidi huo.
4. Je, kuna hoja yeyote ya msingi kutilia mashakautoshelevu wa ushahidi huo.

## KIPIMO CHA MASLAHI YA UMMA

Katika kila kesi, hata kama ushahidi unatosha

kuthibitisha shtaka au kutoa suluhu yeyote mbada la, Waendesha Mashtaka lazima pia wazingatie matakwa ya maslahi ya umma.

Katika kutumia kipimo cha maslahi ya umma wakati wa hatua ya kuamua kuanzisha mashtaka, Waendesha Mashtaka wanapaswa kuzingatiamambo yafuatayo;-

1. Uwepo wa ushahidi wa kutosha na kwa kulinganisha na maslahi ya mwathirika wa tukio na jamii husika.
2. Haki, dira na usawa. Hapa Waendesha Mashtaka wanapaswa kuhakikisha kuwa hakuna ubaguzi kwa misingi ya rangi, mali, dini, elimu,jinsia, asili ya kabila wala misimamo ya kisiasaitaruhusiwa.
3. Athari za mashtaka kwa usalama wa Nchi.
4. Wahakikishe kwamba hakuna rasilimali za umma zitapotea bure katika kutekeleza mashtaka yasiyofaa (Thamani ya pesa).

Hata hivyo, mambo mengine ya kuzingatia yanaweza kuwa:-

1. Je, kosa lilifanyika kwa uzito kiasi gani.
2. Je, ni kiwango gani cha hatia ya mtuhumiwa ... kwa mfano, kiwango ambacho kosa lilipangwa, madhara yanayotokana na kosa husika, na kiwango gani mtuhumiwa amefaidika kutokana na mwenendo wa uhalifu.
3. Ni hali gani na madhara yaliyosababishwa kwamwathiriwa?
4. Je, mtuhumiwa alikuwa na umri gani na ukomavu wake wakati wa kutenda kosa.
5. Kuna athari gani kwa jamii? (vi)Je, mashtaka ni jibu sawia.
6. Je, vyanzo vya habari (ushahidi) vinahitaji kulindwa.

## KIPIMO CHA KUSHITAKI KWASABABU YAUMUHIMU

Kipimo hiki kinaweza kutumika pale ambapo kipimo cha “ushahidi” na kile cha “maslahi ya umma” havijitoshelezi, lakini kwa kuangalia uzito wa kosana mazingira yake, ni muhimu kufungua mashtaka kwa haraka.

**Kipimo hiki kinazingatia yafuatayo:-**

1. Kama kuna hoja za msingi kuonyesha kwambamtuhumiwa ametenda kosa.
2. Ushahidi zaidi unaweza kupatikana kufanikisha kutiwa hatiani kutiwa kwa mtuhumiwa.
3. Uzito au mazingira ya kesi yanahitaji kufanyika kwa maamuzi ya kushitaki haraka.
4. Kuna hoja za msingi zinazoendelea kupinga dhamana na kwa mazingira yote ya kesi ni sahihi kufanya hivyo.
5. Ni kwa maslahi ya umma kufungua mashtaka hayo na kuna matumaini kushinda kesi. Na kuhu su matumaini ya kushinda kesi, itategemea uwepo wa ushahidi wa kutosha, ushahidi halisi na ushahidi shawishi na kama utetezi uliopo unapunguzanguvu ya mashitaka.

## MATARAJIO HALISI YA KUSHINDA KESI

Matarajio ya kushinda kesi yanategemea utoshelevu wa ushahidi upande wa mashtaka kwa kulinganisha na mianya ya utetezi kwa mshtakiwa kama utetezi wake unakanusha

tuhuma husika.

**UCHAGUZI WA SHTAKA WAKATI WA KUPENDEKEZA MASHTAKA**

Mwendesha Mashtaka lazima azingatie miongozo ya mashtaka ikiwa ni pamoja na ile iliyoainishwa katika Mwongozo Mkuu wa Waendesha Mashtaka (PGI).

Pamoja na hayo, Mwendesha Mashtaka lazima achague mashtaka yanayolingana na uzito wa tukio na kiwango cha madhara na kwa kuungwa mkono na ushahidi uliopo, kama vile matumizi ya silaha, asili ya mipangilio ya kosa, jambo lolote linalohusisha rushwa au matumizi mabaya ya madaraka Mwendesha Mashtaka pia lazima achague mashtaka yanayoipatia Mahakama mamlaka ya kutosha kutoa adhabu na amri mbalimbali za baada ya kuisha kwa kesi, lakini pia mashtaka yanayoruhusu amri ya kutaifisha mali kufanyika kama mshitakiwa amefaidika na tukio la uhalifu na maslahi ya umma yametimizwa kwa kuchagua kuendelea na shitaka dogo.

Waendesha Mashtaka kamwe wasiendelee na mashitaka mengi kuliko inavyohitajika, na lazima wazingatie mashitaka yeyote muhimu kadiri kesi itakavyokuwa inaendelea.



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa akisikiliza kwa umakini maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Makosa Dhidi ya Binadamu na Utangamano wa Taifa kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bw. Renatus Mkude juu ya majukumu na huduma mbalimbali za kisheria zinazotolewa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakati alipotembelea kwenye banda la maonyesho wakati wa Uzinduzi wa Kampeni ya Huduma ya Msaada wa Kisheria wa Mama Samia (Mama Samia Legal Aid Campaign) Jijini Dodoma.*



# Dhamana Katika Jinai

Makala

**Peter Mauggo**

Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Uratibu wa Upelelezi

Dhamana ni kitendo cha kupewa uhuru wa masharti kwa mshtakiwa ambaye anasubiri kesi yake kusikilizwa, au rufaa kwa masharti yaliyowekwa na mahakama ili kuhakikisha anafika Mahakamani katika tarehe iliyopangwa.Mtazamo huu umejengwa katika Ibara ya 13(6)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoeleza kwamba, Mshtakiwa hatakiwi kuchukuliwa kama mkosaji wa tuhuma dhidi yake hadi ithibitishwe vinginevyo na Mwendesha Mashtaka mbele ya Mahakama yenye mamlaka kamili.

**KUSIKILIZWA KWA DHAMANA**

Ni wakati wa kusikiliza shauri la maombi ya dhamana lililopo mbele ya mahakama ili kuamua kama dhamana inakubalika kwa masharti fulani au haikubaliki.Maombi yanaweza kuletwa mbele ya Mahakama kwa njia ya mdomo au maandishi.

**AINA ZA DHAMANA**

Kuna aina mbili za dhamana; dhamana ya Polisi na dhamana ya Mahakama

**DHAMANA YA POLISI**

Katika dhamana hii, Mtuhumiwa anapokamatwa au kuzuiliwa na Polisi au chombo chochote cha upelelezi chenye mamlaka ya kipolisi, anaruhusiwa kupewa dhamana wakati uchunguzi ukiendelea ili kama itahitajika baadaye,afunguliwe mashtaka mbele ya mahakama au aachiwe

**DHAMANA YA MAHAKAMA**

Dhamana ya mahakama inaweza kutolewa wakati wa kesi au rufaa inayosubiriwa. Pindi shtaka likifunguliwa, mahakama inayo mamlaka ya kutoa dhamana, isipokuwa pale

ambapo sheria inaelekeza vinginevyo. Mfano mzuri ni pale Mkurugenzi wa Mashtaka anapowasilisha mbele ya Mahakama hati ya kupinga dhamana ingwaje kosa/makosa husika kwenye hati ya Mashtaka yanadhaminika.

**HATUA ZA KUTOA DHAMANA**

Mshtakiwa anapofikishwa mahakamani kwa shtaka/mashtaka yanayodhaminika, anatakiwa kupewa dhamana kwa masharti yatakayotolewa na Mahakama yenye mamlaka kufanya hivyo. Mahakama inawajibu wa kumweleza haki yake. Sheria imeweka taratibu mbalimbali zinazotumiwa na Mahakama katika kutoa dhamana.Mojawapo ni Mshtakiwa mwenyewe au wadhamini wake kusaini hati ya dhamana (surities bond) yenye thamani itakayotolewa na Mahakama. Lengo la wadhamini kusaini hati ya dhamana ni kuwa na uhakika wa upatikaji na uwepo wa Mshtakiwa wakati wa usikilizwaji wa shauri dhidi yake.

**DHAMANA KWA MAKOSA YANAYOSIKILIZWA MAHAKAMA KUU**

Kama mtu anashtakiwa kwa kosa linalosikilizwa Mahakama Kuu, lakini ni kosa linalodhaminika, anaweza kupewa dhamana na mahakama ya chini inayomshikilia kwa wakati huo kabla hajapelekwa Mahakama Kuu. Na kwa makosa ya uhujumu uchumi, utoaji dhamana katika hatua hii huzingatia thamani ya pesa iliyopo kwenye hati ya mashtaka

**DHAMANA WAKATI KESI INAENDELEA MAHAKAMANI**

Mshtakiwa aliyeshtakiwa kwa kosa linalodhaminiwa anaweza kupewa dhamana wakati wowote wa kesi endapo atatimiza masharti yaliyowekwa na mahakama. Hata hivyo, ni muhimu mshtakiwa kufikiriwa suala la dhamana kwa makosa yenye dhamana siku ya kwanza anaposomewa mashtaka kwa sababu ni wajibu wa Mahakama kumuelewesha juu ya haki hiyo.

**DHAMANA INAYOSUBIRI RUFAA**

Kiujumla, hata pale mtu anapokuwa ametiwa hatiani na anatumikia adhabu, anayo haki ya kukata rufaa dhidi ya maamuzi hayo ya Mahakama.Lakini kipindi anasubiri usikilizwaji wa rufaa yake anayo haki ya dhamana.Katika maombi yake ya dhamana mrufani anatakiwa kuithibitishia Mahakama kuwa rufaa yake ina nafasi kubwa ya kufanikiwa pale itakaposikilizwa.Pia dhamana inaweza kutolewa pale mrufani atakapoithibitishia Mahakama kuwa analo tatizo la kiafya ambalo ni hatari kwa wafungwa wengine na kwamba tiba yake ni rahisi akiwa nje ya Gereza au anahitaji kutibiwa nje ya nchi kwa vile tiba ya namna hiyo haipatikani hapa nchini.

Kifungu cha 368(1) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai (CPA) kinasimamia utolewaji dhamana wakati wa kusubiria maamuzi ya rufaa. Pamoja na hayo, Kanuni ya 11(2) ya Kanuni za Mahakama ya Rufaa Tanzania zinatoa mamlaka kwa Mahakama hiyo kutoa dhamana kwa mr ufani anayesubiri hatima ya rufaa yake.

Kifungu cha 29(4) cha EOCCA kinasimamia mamlaka ya kutoa dhamana wakati kile cha 36 cha EOCCA kinasimamia mazingira ya kutoa au kukataa dhamana na masharti ya lazima ambayo mahakama inalazimika kuyaweka wakati wa kutoa dhamana kwa mshitakiwa.

MAKOSA YASIYO NA DHAMANA.

Kwa mujibu wa Sheria mbalimbali za nchi

kuna makosa ambayo yameainishwa ambapo Mtuhumiwa/Mshtakiwa anazuiliwa dhamana. Makosa hayo ni mauaji ya kukusudia,Uhaini, Ugaidi, Unyang'anyi wa kutumia silaha, Utakasishaji fedha ,Usafirishaji madawa ya kulevya na usafirishaji haramu wa binadamu.

**KUTOA AU KUZUIA DHAMANA**

Polisi na Mahakama wana wajibu wa kutoa dhamana kwa watuhumiwa ama washtakiwa kwenye makosa yanayodhaminika. Lakini zipo sababu kadhaa ambazo zinaweza pelekea Polisi wasitowe dhamana.Mahakama kwa upande wake pia , Mwendesha Mashtaka anaweza kuomba zuio la dhamana hata kwenye makosa ambayo sheria inaruhusu dhamana. Sababu hizo ni kama ifuatavyo;

a) Uwezekano wa kutoroka mashtaka yanayomkabili. Vigezo vinavyotumika hapa ni pamoja na uzito au ukubwa wa kosa husika pamoja na ukubwa wa adhabu kama mtuhumiwa akipatikana na adhabu,

b) Uwezekano wa kuingilia na kuvuruga upelelezi na ushahidi ama mashahidi. Hii mara nyingi ni pale upande wa mashataka utakapothibitisha Mahakamani juu ya uwezekano huo. Hisia pekee siyo kigezo cha kupinga dhamana,

c) Uvunjifu wa amani na usalama. Hii ni pale ambapo upande wa mashtaka utaithibishia Mahakama kuwa endapo mtuhumiwa / Mshtakiwa atapewa dhamana anaweza kuendeleza uvunjifu wa amani na usalama wa nchi,

d) Usalama wa Mtuhumiwa / Mshtakiwa. Yapo mazingira ambayo kama mshtakiwa atapewa dhamana , basi usalama wake uko mashakani.Kwa mfano kama Mtuhumiwa au Mshtakiwa ni mhalifu endelevu na jamii yake imemchoka kwa tabia yake ya uhalifu,

e) Usalama wa nchi na Maslahi ya Umma. Katika eneo hili kifungu cha 148(4) Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai Sura ya 20 kinamruhusu Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuwasilisha Mahakamani hati ya zuio la dhamana pale atakapoona inafaa na ni kwa usalama wa nchi na maslahi ya Taifa / Umma. Mara nyingi hii imefanyika kwenye makosa makubwa ya Uhujumu uchumi.

f) Uwezekano wa Mtuhumiwa/ Mshtakiwa kurudia kutenda kosa au makosa mengine ya aina hiyo. Endapo upande wa Mashtaka utaithibitishia Mahakama kuwa Mtuhumiwa akipewa dhamana atafanya makosa mengine au kurudia kutenda kosa linalomkabili, hiyo huweza kuwa sababu tosha ya kuzuia dhamana,

g) Pale ambapo Mtuhumiwa/Mshtakiwa alishtakiwa na kuhukumiwa kifungo kinachozidi miaka mitatu gerezani,

h) Pale itakapothibitiswa na Mwendesha Mashtaka kuwa Mtuhumiwa/Mshtakiwa aliwahi kuvunja masharti ya dhamana kwa kuruka dhamana. Kwa ujumla polisi au Mahakama baada ya kujiridhisha na uwezekano wa kupatikana kwa Mtuhumiwa/Mshtakiwa wanaweza kutoa au kutokutoa dhamana.

Ingawaje dhamana ni haki ya Mshtakiwa, kabla ya kutoa dhamana Mahakama ni lazima ijiridhishe na upatikanaji wa Mshtakiwa wakati wa usikilizaji wa kesi ama uwezekano wa mshtakiwa kuruka dhamana na hivyo

kupelekea haki kutokutendeka

**MASHARTI YA DHAMANA**

Katika utoaji wa dhamana kwa Mshtakiwa Mahakama utilia maanani sheria na maamuzi mbalimbali yaliyokwisha kutolewa kuhusiana na dhamana. Kifungu cha 148(5) cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai kinatanabaisha makosa ya jinai yasiyo na dhamana na katika mazingira gani mshtakiwa anaweza kunyimwa dhamana. Kifungu 148(6) kinaweka bayana masharti Mahakama inapaswa kuegemea wakati wa utoaji wa dhamana. Pamoja na sheria hiyo, pia sheria ya Uhujumu Uchumi na Makosa ya Kupannga sura ya 200 kifungu 36(4) kinaweka zuio la dhamana kama Mahakama itaona inafaa. Lakini kifungu cha 36(5) kinaweka masharti ya Mahakama kuegemea wakati wa kuweka masharti ya dhamana.Kimsingi Sheria hii inasomwa kwa pamoja na Kifungu cha 148(5) na Kifungu148(6) cha CPA.

**MAOMBI YA KUONDOA DHAMANA**

Mdhamini yeyote aliyechukuwa dhamana ya Mshtakiwa anaweza kupeleka maombi yake mbele ya Mahakama akiomba kusitisha dhamana yake juu ya Mshtakiwa aliyemdhamini. Mahakama ina wajibu wa kutoa wito wa kukamatwa kwa Mshtakiwa na kufikishwa mbele ya Mahakama na hatimaye dhamana yake kufutwa. Lakini Mshtakiwa bado ana haki ya kupata dhamana. Pale Mshtakiwa atakapokosa dhamana atapelekwa magereza kusubiria usiklizwaji wa kesi yake. Kama Mshtakiwa ataendelea na dhamana hadi tamati ya kesi na kutiwa hatiani au kuachiwa huru dhamana yake nayo itakuwa imefika mwisho.

**MADHARA YA KURUKA DHAMANA**

Pale Mshtakiwa anaporuka dhamana na kushindwa kufika kwenye shauri dhidi yake, Mahakama kwa njia ya hati ya wito itaamuru wadhamini au mdhamini kufika mbele ya Mahakama kuonyesha kwa nini dhamana alioiweka kwenye hati ya dhamana isitaifishwe kwa sababu ya Mdhaminiwa kushindwa kufika Mahakamani. Mdhamini anatakiwa aonyeshe sababu za msingi na pale anaposhindwa, Mahakama itaamuru ama alipe/walipe kiasi chote cha fedha kama kinavyoonekana kwenye hati ya dhamana au kiasi pungufu na hicho kwa namna Mahakama itakavyoona inafaa. Kama Mdhamini ameshindwa kulipa, Mahakama itaamuru mali zake nyingine ziuzwe ili kulipa dhamana aliyoiweka Mahakamani. Kifungo cha miezi sita(6) Gerezani ni haki ya Mdhamini pale anaposhindwa kutimiza yote mawili hapo juu,



*Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu akizindua rasmi kitabu cha Mwongozo juu ya Ushirikiano wa Kimataifa kwenye Masuala ya Jinai akiwa pamoja na Balozi wa Uingereza nchini Tanzania Mhe. David Concar kwenye hafla ya uzinduzi wa Mwongozo juu ya Ushirikiano wa Kimataifa kwenye Masuala ya Jinai uliofanyika katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es salaam.*



# UTANI WA KISHERIA

## NGURUWE NA MTU

Mrabbi, Mhindu na Mwanasheria walikuwa wanasafiri lakini kwa bahati mbaya gari walilokuwa wanasafiria likaharibika walipofika nje ya mji, na ilikuwa jioni sana, ikawabidi waanze kutembea kwa miguu kuelekea kwenye shamba moja lililokuwa karibu na mahali gari lao lilipoharibikia. Wakamkuta mmiliki wa shamba akawakaribisha na kuwaambia, ni usiku sasa, kwa bahati nzuri nina vitanda viwili vya ziada hivyo itambidi mmoja wenu alale stoo. Yule Mhindu akasema, hamna shida mimi nitalala stoo. Baada ya muda mfupi akaja akagonga kwenye mlango wa ile nyumba walipolala wenzake, mwenye nyumba akafungua, Mhindu akamwambia "Kule kwenye stoo kuna ng'ombe na kulingana na desturi zetu siruhusiwi kulala sehemu yenye ng'ombe. Yule Mrabbi akasema, haya hamna shida mimi nitaenda kulala stoo. Baada ya muda mfupi yule Mrabbi naye akarudi na kugonga mlango, mwenye nyumba akafungua, Mrabbi akasema "Kule stoo kuna nguruwe na kutokana na desturi zetu siruhusiwi kulala sehemu yenye nguruwe. Kwa hiyo, ikambidi Mwanasheria aende kulala stoo, lakini baada ya muda mfupi Mwanasheria pia akarudi na kugonga mlangoni, mwenye nyuma alipofungua akasema, "Ni ng'ombe na nguruwe"

## PATA SIGARA

Mwanasheria mmoja mdogo alikuwa anamtetea mfanyabiashara mahakamani, na akawa na mashaka kwamba atashindwa

kesi, akamuomba mwanasheria mwenzake mzoefu kama anaweza kumletea pakiti ya sigara ili ampe hakimu kama rushwa ya kuhakikisha mteja wake anashinda ile kesi. Yule mwanasheria mkubwa akashangaa! Ha! "Wewe! Hakimu ni mtu wa heshima sana" ukifanya hivyo hautaweza kamwe kushinda hii kesi" akamwambia yule mwanasheria mdogo. Mwishowe, hakimu akatoa hukumu ya kesi ambapo alimpa ushindi mteja wa yule mwanasheria mdogo. Yule mwanasheria mkubwa akasema, "Si unaona, umeshinda kesi bila kuleta zile sigara? Yule mwanashera mdogo akamjibu, "Nilizileta na kuzifunga kwenye kadi ya biashara ya mteja wangu niliyompa hakimu, ndo maana nimeshinda kesi".

## MWANASHERIA MUADILIFU

Mzee mmoja mwenye umri wa miaka 82 aliambiwa na daktari wake kwamba hana muda mrefu wa kuishi tena, atakufa.

Kwa hiyo akaamua kuwaita watu watatu ambao walikuwa wa muhimu sana katika maisha yake, Daktari wake, Mchungaji wake na Mwanasheria wake na akawaambia, "Sina muda mrefu wa kuishi ndo maana nimeamua leo kuwaita kwa sababu ninyi mmekuwa watu muhimu sana kwenye maisha yangu, Ila nataka mnisaidie jambo moja, leo nitawapa kila mmoja wenu bahasha yenye kiasi cha Sh 50,000, tafadhali sana nawaombeni nitakapokufa tupeni hizi bahasha zenye fedha kwenye kaburi langu. Baada ya siku chache yule mzee akafariki dunia, Daktari akasema "Lazima nikiri kwamba nilitumia Sh 10,000 katika fedha alizonipa marehemu kwani nilikuwa ninamdai fedha nyingi kwa ajili ya matibabu yake. Lakini, nilitupa Sh 40,000 ya fedha kwenye kaburi lake." Mchungaji yeye naye akasema, "Lazima nikiri kwamba nilitumia kiasi cha Sh 25,000 alizonipa marehemu kwa ajili ya matumizi muhimu ya Kanisa, lakini nimetupa zilizobaki kwenye kaburi lake kama alivyoagiza," Mwanasheria akasema, siamini hiki ninachokisikia, nawashangaa sana ninyi wawili, mimi niliandika cheki ya fedha zote na kuitupa kwenye kaburi lake,"

## MUDA NA FEDHA

Mwanasheria mmoja alikufa ghafla akiwa na umri wa miaka 45. Akafika katika geti la mbinguni na Malaika aliyekuwa amesimama getini akamwambia "Karibu tulikuwa tunakusubiri kwa muda mrefu" Mwanasheria akamuuliza yule Malaika "Una mana gani? Ndiyo kwanza nimefikisha miaka 45, kwanini nife mapema hivi?. 45? Huna miaka 45 una miaka 82, Malaika akamwambia Mwanasheria. Mwanasheria akamwabia Malaika, subiri kidogo.... nina miaka 45 hata kama ukitaka nitakuonyesha cheti changu cha kuzaliwa. Malaika akamwambia subiri kidogo nikaangalie akaingia ndani. Baada ya muda mfupi yule Malaika akarudi na kusema, Samahani, mbona rekodi zetu zinaonyesha kuwa una miaka 82? Nimeangalia masaa yote uliyowachaji wateja wako, na inaonyesha

una miaka 82.

**ONGEA KUHUSU KIFO MARA TATU**

Siku moja simu ilipigwa katika ofisi flani ya Sheria na mpokeaji simu alipopokea aliyepiga akauliza, naweza kuongea na Dewey? Aliyepokea simu akajibu, “Samahani Dewery amefariki dunia jana. “Oh! Sawa, Kwa heri akasema yule bwana aliyepiga ile simu. Lakini kila siku kwa mfululizo wa wiki mbili yule bwana akawa anapiga simu katika ofisi ile kumuulizia Dewery na anaambiwa hivyo hivyo kwamba Dewery amefariki dunia. Mwishowe alipopiga simu yule mpokeaji simu akaongea kwa sauti ya ukali, Si nimekuambia Dewery amefariki dunia? Sasa mbona unaendelea kupiga simu tu? Yule jamaa akasema, Oh! Kwasababu napenda sana kusikia taarifa ya kifo cha Dewery.



Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Makao Makuu, S.L.P 1733 Dodoma.

# Anuani za Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mikoa

| | | |
|---|---|---|
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 14370<br>Dar es salaam | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 997<br>Songea - Ruvuma | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 6066<br>Morogoro |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 331<br>Mwanza | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 992<br>Bukoba | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 30393<br>Pwani |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S. L.P 3144<br>Arusha | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 321<br>Sumbawanga - Rukwa | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 587<br>Geita |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 199<br>Tabora | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 2401<br>Iringa | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 131<br>Mpanda - Katavi |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 963<br>Dodoma | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 635<br>Shinyanga | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 169<br>Bariadi - Simiyu |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 6433<br>Moshi | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 1073<br>Lindi | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 362<br>Vwawa - Songwe |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 970<br>Mbeya | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 823<br>Musoma - Mara | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 324<br>Tarime |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 418<br>Tanga | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 44<br>Singida | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 39806<br>Temeke |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 174<br>Mtwara | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 498<br>Kigoma | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 6240<br>Ilala |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 165<br>Njombe | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 295<br>Babati - Manyara | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 75601<br>Kinondoni |